Yesu Kristo Yeye Yule
Jana, Leo, Na Hata Milele

Asanteni sana. Mwaweza kuketi. Imekuwa muda tangu nilipokuwa Salem, Oregon, hapo awali. Nami siku zote nimengoja kwa matarajio makubwa nilipoona wakati wa kurudi tena, kupata kuwatembelea watakatifu hawa wa Bwana hapa, wanaokaa Salem na karibu yake.

2 Hatuamini kwamba haya ndiyo makao yenu, kwa sababu hapa hatuna yoyote, bali tunautafuta Mji ujao ambao Mbuni na Mjenzi wake ni Mungu. Kwa hivyo tunakiri kwamba sisi ni wasafiri na wageni hapa, sio wageni sisi kwa sisi, bali wageni katika ulimwengu, kwa sababu urithi wetu ni wa huko juu. Na tulipata majaliwa yapata miaka miwili iliyopita ya kuwatembelea baadhi ya marafiki zetu, hapa Oregon, karibu na Maporomoko ya Klamath, nasi tukawa na wakati mzuri sana.

3 Tunawaletea salamu kutoka kwa watu wengine kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu ambao wanasafiri pia. Na huu ninii wetu . . . mkutano wangu wa tisa mfululizo. Kwa namna fulani ninakuja kwenu kidogo nimechoka, lakini daima niko tayari kumtumikia Bwana katika nafasi yoyote niwezayo.

4 Sasa, tuna mikutano mitano mitukufu iliyoratibiwa, usiku wa leo, na kesho usiku, na kuendelea hadi Jumapili alasiri, nafikiri ni, Jumapili alasiri ndiyo ibada yetu ya kufunga katika huu uamsho. Tunataka kuwashukuru nyote kwa kutuita hapa, huo udhamini, na kwa wote wanaoshirikiana, kwa ajili ya jengo hili la kupendeza, na kila kitu, limejengwa vizuri sana. Nadhani, tukinena kibinadamu, ni kwamba tumefanya kila- . . . mmefanya kila kitu vizuri sana.

5 Sasa, jambo lingine litakalohitaji . . . Kamwe hatuji kuonana, ambalo tulifanya, kwa njia moja, kuonana, lakini hata hivyo tunakuja kumwabudu Bwana, na kujaribu kufanya jambo fulani kwa ajili ya Ufalme Wake. Na sasa, itachukua kila chembe ya juhudi tunazoweza kutoa kulitekeleza. Na itakuwa . . . Sasa, huu ndio mkutano ambao tumeuandaa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, na ni wajibu wa kila Mkristo kutekeleza sehemu yake, kadiri wawezavyo, kuona ya kwamba ni mafanikio makubwa kwa ajili ya Ufalme.

6 Sasa, mara nyingi sisi wahudumu, sisi, na mashirika mbalimbali, na kadhalika, lakini sote tunang'ang'ania Mahali pamoja pakubwa, kila mtu tunayeweza kumwelekeza huko, ndivyo tunavyofanya. Nasi tunajua sasa walei wanayo, pia, nafasi kubwa, sasa, kwao kutekeleza sehemu yao ya

huduma. Kila mmoja wenu hana budi kuwa mhubiri, na hiyo ni, kumwambia mtu mwingine, kuwaingiza wagonjwa na wanaoteseka, kuwaingiza wenye dhambi. Nasi tutapanda Mbegu ya Mungu, na kuomba kwamba Mungu ataimiminia Roho Mtakatifu, na kuleta mazao mengi sana ya watu wakati wa mkutano huu.

7 Hiyo ndiyo nia yetu ya kwanza ni kuwaleta watu; pili, kuwajenga watu wa Mungu, Kanisa; tatu, maombi kwa ajili ya wagonjwa; na kufanya chochote tuwezacho kusaidia kuyaboresha maisha yenu, na kidogo safari . . . mizigo myepesi kidogo.

8 Nasi tunatumai kwamba tutakapoondoka, na mkutano umetawanyika, kutakuwa na . . . mji wote utafaidika, kila mtu, kuufanya kidogo . . . mahali ambapo ni rahisi kidogo kutenda haki, vigumu kidogo kufanya mabaya. Hayo ndiyo tunayotaka kuacha, hayo, tutakapoondoka humu mjini.

9 Tunataka kuripoti, kote kote pwani, katika mikutano hii ambayo tumekuwa nayo huku imekuwa mitukufu. Bwana ametubariki, hayo maeneo yalijaa watu, na tumeona mikutano miwili, mikutano miwili ya mwisho ilikuwa karibu kabisa, kila kiti cha magurudumu, waliokuwa kwenye machela, chochote kile, walikombolewa na—na Bwana, karibu kila mtu aliyekuja mkutanoni. Tulishukuru sana kuripoti hilo kwa wale ambao wanatafuta uponyaji wao wenyewe na wapendwa wao. Na pia kwamba wengi wameokolewa, na kujazwa na Roho Mtakatifu, na makanisa yamebarikiwa. Nasi tunapojisikia, tukifanya hivyo, tunajisikia ya kwamba tunatoa sehemu yetu ndogo kuusaidia Ufalme wa Mungu. Nasi tuko hapa, ndugu, pamoja nanyi ndugu hapa, ninathamini wema wenu wa kunialika hapa, na kuwa nami hapa.

10 Nami nimekuja sasa ku—kufanya hivi: Yesu alisema, "Ufalme wa Mbinguni umefanana na mtu aliyechukua wavu, akaenda baharini. Naye akauvuta huo wavu, na kile alichokamata . . . " Sasa, najua kwamba kila mmoja wenu, katika makanisa yenu, ana wavu, nawe unauzungusha tu kwenye eneo lako kujaribu kukamata kila samaki uwezaye. Sasa, nimekuja kupanda wavu wangu pamoja na zenu nyote, nasi tutafikia mbali sana, kote mjini, kila mahali, tuone kama hatuwezi kuvuta ndani kitu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Hilo ndilo lililotuleta hapa, kufanya kila tuwezalo ku—kusaidia.

11 Sasa, ni, nafikiri kimsingi haina mipaka ya kimadhehebu, kila mtu amekaribishwa, Mprotestanti, Mkatoliki, Myahudi, yeyote yule, mwenye dhambi, mtakatifu, mtu yeyote, hata kwa mlevi kama atajiheshimu na kutulia. Amekaribishwa tu kuja kama mtu yeyote yule, lakini hana budi kujiheshimu, inampasa kuiheshimu nyumba ya Bwana.

12 Tunashukuru kwa ajili ya ghala hili la silaha, au meja, au yeyote yule ambaye alituruhusu kuchukua jengo hili zuri, nafikiri linapendeza. Nilikuwa hapa leo nikilitazama, nikijaribu kusikika kwa sauti, na kuongea, na pande zote ni kamilifu kabisa. Basi mnaweza kunisikia vizuri kila mahali sasa?

13 Mnajua watu, ni ya hewani, na kidogo ni vigumu sana unapochukua jengo tupu na kuzungumza, halafu kulijaza watu hilo jengo na kuongea, ni tofauti kabisa. Na kwa hiyo sasa wakati mwingine katika kuzungumza mimi hupaza sauti kidogo, kwa sababu mimi ni mwinjilisti, mmishenari, nami nimezoea kuhubiri kwenye mbuga tu, au uwanja wa michezo, huko nje, ambako wakati mwingine huna kipaza sauti, inakulazimu tu kupiga makelele kana kwamba unawapigia ng'ombe kelele, lakini silimaanishi hivyo, nami ni—nina hakika mtaelewa.

14 Na sasa, kwa kawaida usiku wa kwanza wa mkutano kidogo ni usiku mgumu, kwa sababu kila mtu anajaribu kumzoea mwenzake. Na—na wengine wako chini ya matarajio, wengine wanashangaa, na wengine hawajawahi kuwa mkutanoni hapo kabla, na wengine wamesikia, na—na halafu wanatoa maoni yao. Jambo la kwanza mhudumu analosema kwa kawaida hukubalika kwa mtu fulani, wengine hawataki uhusiano wowote nalo, na inakubidi kukabiliana na hayo yote.

15 Lakini hebu tusituhumiane. Ninaamini kwamba ninyi ni watoto wa Mungu, ninawatakeni mniamini kuwa vivyo hivyo, ya kwamba mimi ni ndugu yenu, nami niko hapa kuwasaidia. Sasa, mimi—mimi ni mkusini na—nami sijaachana na usemi wangu bado, wa kuwa mpole kidogo, ingawa nimetembea sana. Kwa hiyo nivumilieni, kwa sababu siwezi kuliwazia upesi sana, mnajua, na inanibidi tu kumngoja Yeye aniambie. Na kwa hiyo nivumilieni, niombeeni, nami nitafanya vivyo hivyo, kuwaombea.

16 Sasa, niliwazia, usiku wa leo, tuna ujumbe mdogo wa utangulizi ambao kwa namna fulani tunatanguliza mkutano kwake, mazungumzo mafupi tu ya kawaida. Na hivyo kidogo tunapata kufahamiana, ku—kujuliana hali, ndipo basi tunatulia mkutanoni.

17 Na sasa, nawatakeni mnifanyie jambo hili, ninawatakeni kuninii . . . Kuna . . . Tunavyo vingi, viti. Kwa kawaida, katika mikutano ambayo tumekuwa tukifanya, kotekote kuanzia kwenye Ikulu ya Ng'ombe kwenda juu, kumekuwako na watu wasingeweza kupata kiti. Mahali pa mwisho tulipokuwa walikuwa wamesimama, napo mahali hapo palikuwa pamejaa saa kumi na moja alasiri, usingeweza kupakaribia. Na kwa hiyo sasa, tuna viti vingi.

18 Na—nami najua watu hapa Oregon huenda kanisani, nao ni watu wazuri. Nao watu wa Mungu kila mahali ni wazuri. Nasi tungependa kuona, tekeleza sehemu yako sasa kwa Ufalme wa

Mungu, kwa sababu hilo jukumu kwa jumla si la wachungaji wenu au juu yangu mimi, ni juu yetu sote kumheshimu Mungu. Na sasa, itekelezeni sehemu yenu, tutatekeleza yetu na mambo ya kati, ninaamini litakuwa jambo kubwa, na hilo ndilo tunalotazamia.

19 Ninaamini katika Kuja kwa Bwana Yesu, ninaamini kurudi kimwili kwa Kristo. Ninaamini kumekaribia sana, ninaamini tumekaribia wakati huo sasa. Sasa, hakuna ajuaye wakati atakapokuja, si hata Malaika. Alisema ni Baba pekee ajuaye hilo. Kwa hiyo basi, hatujui, lakini tunazo ishara ambazo tunatazamia, kujua kwamba mambo haya yatakapoanza kutokea, wakati unakaribia. Kwa hiyo bila shaka tunaweza kuona baadhi ya ishara kuu sana za kusadikisha sasa, kwamba—kwamba wakati umekaribia.

20 Na kwa hiyo naamini ufadhili huu ni wa ndugu wa Kipentekoste, mimi ni mmoja pia. Lakini tunataka mjue ya kwamba Pentekoste hiyo, kwenu ninyi Methodisti, Baptisti, na Mpresbiteri, tunaamini ninyi ni Wapentekoste pia. Mnaona, Pentekoste sio dhehebu, Pentekoste ni tukio ambalo sote tunaweza kupata. Mnaona? Iwe wewe ni Mkatoliki, au Mbaptisti, au Mpresbiteri, chochote kile, Pentekoste ni tukio, na ni kwa yeyote atakaye. Hiyo ni kweli. Na ni kila mtu. Ninao wengi sana . . .

21 Nilitoka katika kanisa la Kibaptisti, ningali nina ushirika, mikutano ya ajabu kwa ajili yao, na nina Episkopalia, Presbiteri, mwanzoni msingi wa familia yangu ni Katoliki, mimi ni Mwairishi. Na kwa hiyo kupitia hapo Mungu hajawahi kumhoji mtu yeyote jukwaani, ninapowaombea, "Sasa, itabidi ubadilike kutoka Methodisti hadi Baptisti." Hilo silo wazo.

22 Mnajua, mimi ni mzee, nina umri wa miaka hamsini na mitatu, nami nimekuwa pamoja na familia ya Branham miaka hii yote, nanyi mwajua, hawajawahi kuniomba nijiunge na familia hiyo, ajabu, lakini ninaamini nilizaliwa nikiwa wa Branham. Na kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyoamini sisi ni Wakristo. Mnaona? Tu—tu—tunawazia unapaswa kujiunga na kanisa fulani na kuwa na ushirika, lakini kwa kweli, kuwa Mkristo ni kuzaliwa Mkristo, tukio la kuzaliwa mara ya pili la kuwa Mkristo.

23 Na sasa, hebu tena, kabla sijachukua somo, ni kusema tunawaombea wagonjwa. Sasa, huenda kuna madaktari walioketi hapa karibu. Daktari, sikuja kumchukua mgonjwa wako, naja kumwombea mgonjwa wako. Unaona? Ni—ninaamini ya kwamba uponyaji wa Kiungu umekuwa mojawapo ya mambo yaliyopuuzwa sana halafu, kumekuwa na mengi sana pia juu ya uponyaji wa Kiungu ambayo yameenezwa chini ya jina la uponyaji wa Kiungu, ambayo hayakupaswa kuenezwa, tu—tunatambua hilo. Kanisani, wokovu, mwingi umeenezwa, loo,

kwa namna fulani dini ya kiakili, kwamba ujiunge tu na kanisa kama vile chama, na kuachilia yote. Hatuamini hilo. Tunaamini huna budi kuzaliwa mara ya pili, tunaamini huna budi kuwa Mkristo kwa kuzaliwa.

24 Nami ninaamini kuna mambo mengi yameenezwa chini ya uponyaji wa Kiungu, himaya ya uponyaji wa Kiungu, au unaoitwa hivyo, na ingeninii . . . kungekuwa na kila kitu isipokuwa uponyaji wa Kiungu, hisia za kila namna, na—na kadhalika.

25 Lakini nitajieleza dhahiri, na haya yanarekodiwa, kwamba ninaamini kwamba kila baraka ya ukombozi inayoiendea jamii ya wanadamu imeshalipiwa tayari, na ni mali yako, kwamba "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tulipona." Ni wakati uliopita. Ninaamini kwamba wakati Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alipokufa pale Kalvari, alinunua wokovu wetu, na kila dhambi duniani ililipiwa.

26 Sasa, hautakufaa kitu mpaka uukubali kama mali yako binafsi. Lakini ukijaribu kusema tu, "Naam, Yeye husamehe dhambi," naam, rehema ya Kristo, mauti ya Kristo ilifanya upatanisho kwa ajili ya dhambi, "Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu," bali huna budi kumkubali kama Mwokozi wako, la sivyo kamwe haitakufaa kitu.

27 "Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Kwa hiyo, hakuna mtu ambaye angeweza kumwokoa mtu wala kumponya mgonjwa, tayari imekamilika pale Kalvari. Ninaamini Kalvari ililipa hiyo gharama, Yesu Kristo pale Kalvari alilipa hiyo gharama.

28 Sasa, ninaamini kama ungekuja chini ya mafundisho ya mchungaji wako, na kumwamini Bwana Yesu, na kumkubali kama Mwokozi wako, ninaamini utaokolewa. Hiyo ni kweli. Nami naamini ya kwamba unapolisikia Neno la Mungu likihubiriwa, na kusema ya kwamba Hilo ndilo . . . ya kwamba alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tulipona, nawe utalikubali kwa misingi hiyo, hivyo ndivyo inavyofanywa. Kwa maana Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayetuombea tunapoungama.

29 Mnaona, kwanza tunakubali, na kukiri Yeye amelifanya, ndipo basi anaweza kwenda kufanya kazi katika ukuhani Wake mkuu kama Kuhani Mkuu wa kutuombea tunapokiri yale aliyotufanyia pale Kalvari. Hiyo—hiyo imekubalika, sivyo, ndugu? Naam. Mnaona, kwamba Yeye . . . kwamba yale aliyotufanyia pale Kalvari, kwanza tunayakubali, tunayakiri, na basi Yeye ndiye Kuhani Mkuu kutimiza yale tunayokiri Yeye amefanya. Mnaona? Hiyo ni kwa ajili ya uponyaji au wokovu.

30 Sasa, ninaamini ya kwamba Mungu anaweza kufanya lolote analotaka kufanya, kwa sababu Yeye ni Mungu, bali ninapenda hilo litoke tu katika Biblia, ndipo najua niko sawa. Ninaamini

Biblia kuwa ni Neno la Mungu lisiloweza kukosea, siamini kwamba Hilo linapaswa kuongezewa wala kuondolewa.

31 Sasa, kama mtoto, mvulana mdogo, mama na baba wote Waairishi, nilipouhisi huo wito wa Mungu, nilishuka kwenda kanisani, naye kuhani akaniambia kwamba wokovu uko kanisani. Vema, ndipo nikaja kujua kutoka kwa marafiki zangu waliokuwa wa makanisa mbalimbali, ni kanisa gani kati ya hayo lina wokovu ndani yake basi? Mnaona? Kama Katoliki ingekuwa sahihi, basi Lutheri hakika imekosea; kama Lutheri ni sahihi, basi kuna kasoro kwa Wabaptisti. Kwa hiyo ni lipi kati ya makanisa hayo lingekuwa sahihi?

32 Baada ya kutafuta, nikijaribu kujua, kuchambua, na chochote ningeweza kufanya, nilikuja kugundua ya kwamba Mungu yuko ndani ya Neno Lake, nalo Neno ni kweli. Mungu hatauhukumu ulimwengu kwa kanisa, bali kwa Neno, kwa maana naona katika Kitabu cha Ufunuo lilisema, "Yeyote atakayeondoa Sehemu moja au kuongeza chochote Kwake, huyo ataondolewa sehemu yake kwenye Kitabu cha Uzima." Na basi naamini halina makosa, ya kwamba halina budi kuwekwa jinsi tu lilivyoandikwa.

33 Ninaamini si la kutafsiriwa apendavyo mtu. Ninaamini ni. . .Mungu amelilinda, na ndilo njia hasa, ambayo Yeye atauhukumu ulimwengu, kwa Kitabu hiki. Sasa, hana budi kuwa na kigezo, mahali fulani, kuuhukumia ulimwengu. Kwa hiyo kanisa litahukumiwa kwa Neno.

34 Hivi ndivyo na—nafikiri haliwezi kukosea: Haliwezi kukosea sana, hata wakati Hawa, si kutokuamini, bali kusikiliza hoja ndogo dhidi Yake, alisababisha kila kifo, na kila huzuni, na kila huzuni kubwa. Hivyo ndivyo alivyofanya.

35 Ninaamini ya kwamba mke wa Lutu, kama alivyoamriwa na Malaika asiangalie nyuma, naye akageuka na kuangalia nyuma, naye amesimama leo, nguzo ya chumvi, kwa sababu alikosa kuliamini tu Neno la Mungu kiasi hicho. Sasa, alikuwa na sababu nzuri kuliko tuliyo nayo mimi na wewe. Unaona, watoto wake, na wajukuu wake walikuwa wakiteketea katika Hukumu za Mungu. Na vilio vya watoto wake mwenyewe, na wajukuu wake, na moyo wa mama ukilia uliasi Neno la Mungu vya kutosha kutazama juu ya bega lake, na hapo akageuka.

36 Mnaona, ninaamini Neno halina budi kuwa jinsi hasa lilivyoandikwa, hivyo tu. Je, mtaliamini pamoja nami? Juu ya msingi huo, hebu na tujitulize sasa kwenye Neno na kunena juu ya Neno. Na tuombe sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu.

37 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hakika kuna haja nyingi humu jengoni. Kwa uaminifu mbele za Mungu, kama una haja ambayo ungependa Mungu atimize, wakati wa mkutano huu, inua mkono wako Kwake sasa na useme, "Kwa jambo hili,

Mungu, nataka unikumbuke. Nina mpendwa ambaye anataka kuokolewa. Nina maradhi, ama kitu fulani."

38 Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia Kiti Chako cha neema. Hatungetaka kukikaribia Kiti cha haki, kwa kuwa tusingeweza kusimama hapo; tusingeweza kukikaribia Kiti cha Hukumu, tusingeweza kusimama hapo. Kwa haki, tunapaswa kuhukumiwa kwa sababu sisi ni wa ulimwengu, jamii iliyoaguka ya Adamu, bali tunakikaribia Kiti cha rehema.

39 Naye Yesu, alipokuwa duniani, alisema, "Mkimwomba Baba neno lolote kwa Jina Langu, mtapewa." Nami ninaomba sasa kwanza, Bwana, msamaha wa makosa yetu yote dhidi ya amri Zako, utusamehe, Bwana, kila mmoja. Tunawaombea ndugu zetu wahudumu, kwa ajili ya kusanyiko lao, kwa ajili ya dhambi za mji, na za taifa, za watu kila mahali.

40 Mungu, ninaomba kwa ajili ya dhambi yangu mwenyewe, nasi tunajua kwamba dhambi kiasili ni kutokuamini. "Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari." Na kutokuamini ndiko kunakotufanya tutende makosa ya uovu tunayotenda, na kama tu tukiamini, hatungefanya mambo hayo. Kwa hiyo naomba, Baba, ya kwamba utusamehe kutokuamini kwetu, na utakuja kwa kila mmoja wetu usiku wa leo, na utupe imani ambayo itajibu ombi tulilo nalo chini ya mikono yetu, tujalie, Bwana, hilo liko moyoni mwetu.

41 Tumekuja hapa kwa kujisikia kuongozwa na Roho Wako. Shetani alitupiga vita, kujaribu kutuzuia tusije, lakini hiyo ndiyo sababu naamini zaidi kwamba kuna kitu tulichowekewa akiba. Nasi tunapiga vita usiku wa leo, na Wewe umefungua njia.

42 Sasa, Baba, jalia sote tupate ono hili na tukumbuke yale tuliyoomba, na hapo tusonge mbele na ombi letu. Nami ninaweka langu juu ya madhabahu ya dhabihu usiku wa leo, maombi yangu, imani yangu, yote juu ya madhabahu Yako ya dhahabu ambapo Dhabihu yetu, Kristo, imewekwa pamoja na maombi na mahitaji ya watu hawa wote. Na kwa pamoja tunaomba kumiminwa kukubwa kwa Roho Wako. Bwana, fanya mambo ya ajabu sana kuliko yote tuwezayo kufanya au kuwazia. Jalia imwagwe juu ya mkutano huu, Bwana.

43 Na utakapokwisha, jalia kuwe na uamsho wa mtindo wa kale utakaozuka kote humu nchini, na makanisa yote yawake moto kwa ajili ya Mungu, watu wakiokolewa, na watu kuponywa, na utukufu kuletwa kwa Ufalme wa Mungu. Juu ya ombi hili, pamoja na haya mengine yakiwa juu ya madhabahu Yako ya dhahabu, tunaomba juu yao Jina la Yesu Kristo, kwamba utatujibu sawasawa na rehema Zako kuu. Amina.

44 Msisahau kila ibada. Nami naamini ya kwamba mwanangu aliniambia, nilipoingia huko nyuma hapa nje, kwamba kulikuwa na kiamshakinywa cha wahudumu asubuhi. Hiyo ni kweli? Asubuhi. Sawa kabisa, si—sikuzote napenda kukutana na ndugu

zangu na—na kupata kuzungumza nao kwa muda kidogo, na kufahamiana, na kufahamiana upya. Na sasa, kila mtu akumbuke sasa, hebu tutekeleze sehemu yetu.

45 Na sasa, sijui ni saa ngapi nyinyi watu kwa kawaida hufunga ibada zenu hapa. Na wakati mwingine. . . Mimi ni mmishenari, na kwa kawaida inatubidi tu kuliingilia tunapoweza na kukaa muda mrefu tuwezavyo. Na—nami nimekuwa nikiwachelewesha watu kidogo, si kama nifanyavyo ninapokuwa nyumbani.

46 Nilikuwa nyumbani kwangu hivi majuzi, nami natumaini siwashtui, nilihubiri kidogo, ibada fupi, saa sita. Lakini hiyo ilikuwa fupi tu. Lakini. . . Na lakini, sababu ya kutumaini sitafanya hivyo hapa, lakini kwa kawaida kama dakika arobaini na tano, ama kitu kama hicho, kisha tunaninii. . . kama tutakuwa na mstari wa maombi. Na kwa hiyo sasa, niombeeni sasa tunapofunga sasa, kwa ajili ya Neno.

47 Sasa, huu ni ujumbe mdogo tu wa kawaida ambao kwa kawaida tunawekea msingi usiku wa kwanza, halafu kutoka hapo na kuendelea ndipo tunaona yale ambayo Bwana atatujalia.

48 Katika Yohana Mtakatifu 12:20 tunasoma maneno haya:

> *Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwao waliokwea. . . sikukuu:*
>
> *Basi hao walimwendea. . . Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwomba, wakisema,* Mabwana*, sisi tunataka kumwona Yesu.*

Yohana Mtakatifu 12:20. Katika Waebrania mlango wa 13 na m—mlango wa 13 na ki—kifungu cha 8:

> *Yesu Kristo yeye yule jana, . . . leo, na hata milele.*

49 Sasa, hilo hapo tamshi kuu: *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele.* Sasa, Wayunani hawa walikuwa na njaa tu kama mtu yeyote yule. Shauku yao, walikuwa wamesikia habari za Yesu nao walitaka kumwona Yesu. Wala siamini kwamba mtu yeyote anaweza kusikia habari za Yesu pasipo kutamani kumwona. Hiyo ni kweli? Sasa, nikisema jambo fulani nawe useme, "Amina," hiyo haitanitisha hata kidogo, itanitia moyo. Sasa, ni wangapi hapa wangependa kumwona Yesu? Hebu tuone mkono wako. Tungependa kumwona.

50 Sasa, kama vile ndio kwanza nitoe matamshi yangu, ninaamini Neno kuwa ni Kweli. Sasa, hawa Wayunani walikuja wakitamani kumwona Yesu, nao wakapata kumwona, kwa mmoja wa watumishi Wake. Vema sasa, ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, nasi tunatamani kumwona, vipi kuhusu hilo? Hmm? Mnaona? Hapo inaweka Neno la Mungu kwenye shindano la kuamua. Mnaona?

51 Kama tunatamani kumwona, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, na mmoja wa watumishi wa Mungu akawaleta

Wayunani hawa Mbele za Yesu, basi tunapaswa kuwa na jambo lile lile leo, kama Yeye ni yule yule. Sasa, tunaamini jambo hilo, ya kwamba Yeye ni yule yule kama alivyokuwa wakati huo.

52 Sasa, tungemjuaje kama tungemwona? Sasa, kama tungesema, "Vema sasa, angezipiga wei vipi nywele Zake? Je, alikuwa na mawimbiwimbi marefu yakining'inia kwenye mabega Yake? Je, alikuwa na nywele nyekundu? Je, zilikuwa za shaba? Je, alikuwa na nywele kweli? Alikuwa na upara? Alikuwa—alikuwa na macho ya bluu, macho ya kahawia? Alikuwa mtu mkubwa, mtu mdogo?" Mbona, tunajadili hilo saa zote, na kila mmoja ana maoni tofauti. Kwa hiyo hatungeweza kukubaliana kwa misingi hiyo.

53 Vema basi, vipi kama ningesema tutoke twende hapa nje mjini usiku wa leo, nasi tungemwona mtu ambaye kwa kweli tungeweza kuona makovu ya misumari mkononi mwake, mikono yote miwili, na alama za miiba *hapa*, na kovu ubavuni mwake, chini tu ya moyo wake, naye angekuwa amevaa joho, na—na kutimiza vipimo vyetu? Bado hiyo inaweza kuwa kwamba . . . Kwa kweli, kama tungemchukua mtu kama huyo, haingekuwa ni Yesu. Katika Kuja Kwake Mara ya Pili, kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri. Basi mwili Wake wa kawaida utakaporudi duniani, itakuwa kama jua linavyoangaza kutoka mashariki hadi magharibi. Mnaamini hilo? Hakika. Haingekuwa.

54 Je, tungemjuaje Yesu basi? Jinsi ninavyowazia kwamba tungemjua Yeye ingekuwa kwa asili Yake, kile alichokuwa. Sasa, nikianza kuuliza, "Je, Baptisti wanaamini ni kanisa lao? Presbiteri?"

"Naam."

"Katoliki?"

"Naam."

"Protestanti? Kwa hiyo . . . Myahudi?"

55 "Naam." Au nini . . . Sio Wayahudi, bila shaka hawaamini katika Bwana Yesu kuwa Mwana wa Mungu. Lakini ndugu zetu mbalimbali wa Kipentekoste, madhehebu yao mbalimbali, wangesema, "Naam, iko katika letu." "Iko katika letu," na kadhalika. Lakini sasa, hebu tuseme hilo ni sawa, hiyo iko katika hayo yote. Hebu tuamini tu.

56 Lakini sasa, hakika, kuna tofauti nyingi sana hata kunapaswa kuwa na njia fulani ya kutangaza, hakika, alicho Yeye, mnaona, kwa maana Biblia ilisema Yeye ni yule yule.

57 Kwa hivyo mmoja wao anasema, "Tunaamini katika kukariri . . . kurudia maombi." Huyo mwingine ana Doksolojia; huyo mwingine ana kanuni fulani ya imani wanayotumia. Mmoja anasema, "Ninaamini kama ukinena kwa lugha huyo atakuwa Ndiye." Mwingine akasema, "Ninaamini ukicheza

katika Roho huyo atakuwa Ndiye." Nasi tuna mihemuko ya kila namna na chochote kile.

58 Lakini, halafu basi katika hilo kuna ubishi mwingi, mmoja atasema, "Vema, siamini unafanya *hivi*," na huyo mwingine anasema, "Si . . ." Lakini panapaswa kuwepo na njia fulani ambayo tunaweza kufikia mahali pa kujua, hasa, Yeye ni Nani na Yeye ni Nini. Mnaona, panapaswa kuwepo na mahali fulani. Mnaona?

59 Mmoja anasema, "Naam, nilipaza sauti," mwingine anasema, "Nilicheza katika Roho," huyo mwingine anasema, "Nilinena kwa lugha." Mambo hayo ni mazuri, yote ni mazuri. Lakini hata hivyo, mnaona, husababisha u—ubishi. Mmoja anasema, "Nilimpokea *hivi*," mmoja anasema, "Nilimpokea nikilia," mwingine anasema, "Nilimpokea kwa mizizimo, mtetemeko," mwingine anasema, "Niliona nuru," na huyo mwingine . . . Unaona, kuna tofauti kubwa, kunapaswa kuwe na njia fulani ambayo tungejua kwa hakika, kusudi kusiwe na swali akilini mwetu. Na Biblia ilisema Yeye ni yule yule, kwa hiyo kunapaswa kuwe na njia fulani ya kujua. Sivyo? Nafikiri kunapaswa kuwa na njia fulani ya kujua.

60 Sasa, siamini ya kwamba Biblia ilisema mambo hayo, na kufanya ahadi hizo bila kuweza kuzitimiza. Je, huamini hilo? Ibrahimu, ambaye sisi ni Uzao wake, "Ikiwa tuko ndani ya Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu," naye Ibrahimu alishawishika kabisa, Warumi 4, ya kwamba Yeye angeweza ku—kuweka, au kutekeleza, yale aliyoahidi kufanya. Na kama Mungu akitoa ahadi wala hasimami nyuma yake, basi Yeye si Mungu. Na kama akitoa ahadi, Yeye anaweza kusimama nyuma yake la sivyo hangetoa ahadi kamwe.

61 Sasa, mimi—mimi nina kikomo, na Yeye hana kikomo, kwa hiyo hawezi kukosea, mimi naweza, wewe unaweza, ndugu zetu wanaweza, sote tunaweza kukosea, tuna kikomo. Leo, kama sijui zaidi ya nilivyojua mwaka jana, sipigi hatua yoyote, lakini Mungu hawezi kuendelea mbele, kwa sababu kwanza kabisa Yeye ni mkamilifu, na kila uamuzi ni mkamilifu.

62 Sasa sikilizeni, kama Mungu akiwahi kuitwa jukwaani kufanya uamuzi, akiisha kufanya uamuzi huo ambao unalitatua Milele, kamwe hawezi kurudi nyuma na kusema, "Nilikosea hapo." Na kama hatatenda, kila wakati, jinsi alivyotenda mara ya kwanza, Yeye alitenda vibaya mara ya kwanza. Mnaona, Yeye ni mkamilifu. Kwa hivyo akiitwa kamwe ku—kufanya jambo lolote, na mara uamuzi Wake unapofanywa, huo umemalizika daima, Milele.

63 "Mbingu na nchi zote zitapita, lakini Neno hilo kamwe haliwezi kushindwa," kwa sababu ni sehemu ya Mungu. Mnaliona? Hivyo basi angalieni, Mungu alipoitwa jukwaani kumwokoa mtu aliyepotea, njia Yake ya kwanza ya kumleta

mtu huyo kwenye wokovu ilikuwa ni kwa damu, hajawahi kuibadilisha.

64 Watu wanaokolewa tu . . . Kuna mahali pamoja tu pa ushirika pamoja na Mungu, na hapo ni chini ya damu iliyomwagika. Haijawahi kuwa kwa kanuni za imani, haijawahi kuwa kwa kanisa, haijawahi kuwa kwa dhehebu, haijawahi kuwa kwa taifa, ni kwa damu. Israeli walikutana chini ya damu iliyomwagika, na kote katika wakati, nasi bado tunakutana chini ya Damu iliyomwagika, tusipofanya hivyo, hatuwezi kuwa na ushirika. Hiyo ni kweli.

65 Sisi . . . Ushirika unarejeshwa tu kwa Mungu kwa njia ya Damu, kwa maana jamii ya wanadamu inaweza tu kukutana na Mungu wakati Dhabihu ya Damu imesimama pale kwa ajili yake. Amina. Hilo linatupa hakikisho, uzima, si jambo fulani la kubuni ambalo limetabiriwa katika siku za mwisho hapa, kila kitu kitakuja . . . karibu, na mambo ya kila namna. Lakini tunaamini Neno kuwa ni Kweli ya Mungu, kwa hiyo halitashindwa kamwe. Na uamuzi wa kwanza wa Mungu ulikuwa ni kumwokoa mtu kwa damu iliyomwagika, na Yeye angeninii . . . kila mtu ambaye amewahi kumjia Mungu amepitia njia iyo hiyo kila wakati.

66 Na masharti ya Mungu kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu yalikuwa juu ya msingi wa imani, na hivyo ndivyo anavyowaponya usiku wa leo, ni juu ya msingi wa imani. Haijalishi jinsi mtu alivyo mashuhuri . . . Ikiwa Kristo, Mwenyewe, angekuwa amesimama hapa, mimbarani, amevaa suti hii aliyonipa, kama angalikuwa amesimama hapa amevaa suti hii, asingeweza kukuponya, hata kidogo; tayari amefanya hivyo. Anaweza kufanya kitu kukusadikisha, au kukuelekeza kwenye Neno, na hilo lingekuwa la kusadikisha, na huenda akakuonyesha kupitia karama fulani ya Kiungu kwamba Yeye alikuwa Kristo, lakini asingeweza kukuponya, kwa sababu amekwisha kufanya hivyo.

67 Unawezaje kukomboa kitu chochote kikiisha kukombolewa? Amina. Hiyo . . . Mnaona ninachomaanisha? Ikiwa ukombozi umekamilika, umekamilika. Kama ningekuwa na kisu changu hapa chini kwenye duka la rehani, nami nikanunua hicho kisu tena, na kulipa gharama, na—na nikapata tiketi, basi mtu huyo atanilipishaje tena? Nina risiti yake mwenyewe, tayari kimekombolewa.

Nasema, “Ninataka kukomboa kisu changu.”

“Unayo risiti mkononi mwako.” Loo, jamani!

68 Basi mwanamume au mwanamke yeyote anapomjia Kristo katika utimilifu wa hakikisho la kufa, kuzikwa, na kufufuka Kwake, na ni mfadhiliwa wa kila baraka za ukombozi ambazo Yesu alikufa kwa ajili yake, naye ni . . . Yeye hukupa kitabu cha hundi kilichoandikwa Jina la Yesu chini ya kila moja

yazo, “Mwombeni Baba jambo lolote kwa Jina Langu . . . Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo nanyi mtatendewa.” Hupati tu . . . Unaogopa kutoa pesa kwa hundi, usifanye hivyo.

69 Mara nyingi nimesema ninakutana na matabaka mawili ya watu, katika nyakati zangu kote ulimwenguni, katika kazi ya misheni. Ni—ninakutana na matabaka mawili ya watu, moja ni la Kipentekoste, lingine ni la kimsingi. Wa kimsingi anajua mahali hasa anaposimama, anapachukua kwa Neno, “Mimi ni mwana wa Mungu kwa maungamo yangu.” Mnaona? Anachukua mahali hapo kwa msimamo huo, bali ha—hana imani na yale anayozungumzia. Mpentekoste ana imani nyingi, lakini hajui anaposimama, hajui yeye ni nani.

70 Ni kama vile mtu ana pesa kwenye benki, naye hajui jinsi ya kuandika hundi, naye huyo mwingine anaweza kuandika hundi, huku hana pesa kwenye benki. Laiti ungaliweza kuwaweka hao wawili pamoja! Kama ningeweza kupata imani ya Kipentekoste na—na—na fundisho la kimsingi, au—au vinginevyo, kuwafanya Wapentekoste watambue wao ni nani! Wao ni wana na binti za Mungu, wamekufa tayari, wakazikwa, wakafufuka tena, nao wameketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, si “Utakuwa.” “Ndivyo ulivyo.”

71 Wakati mwingine nafikiri . . . Hivi majuzi ilitokea niligusia jambo linalosikika la kilindi sana kwangu, na ni kwa nadra sana ninafikia jambo lolote ninaloelewa. Lakini nilikuwa nikiwazia, kabla sijalifikia hili, kile ninachojaribu- . . . nitakachojaribu kuwaambia, nilikuwa nikiwaza kuhusu Israeli huko Misri. Nao walikuwa watumwa, na hata hivyo walikuwa ni watoto wa Mungu. Sote tunajua hadithi hiyo.

72 Nao . . . Kama wangewatupia mkate uliooza, iliwabidi kuula, kama waliwabaka binti zao, kama waliwaua wanao, ama chochote walichofanya, kilitendeka tu, walikuwa watumwa. Na hata hivyo hao walikuwa ni wateule, waliochaguliwa na Mungu, wakiwa na ahadi inayongoja hadi wakati wa kutimizwa. Lakini ikaja siku, walikuwa wameenda mbali sana nayo, hata hawakuitambua, hawakujua wakati ulipofika; lakini Mungu sikuzote hachelewi.

73 Sasa, hiyo ndiyo shida ya Wapentekoste siku hizi, hawatambui ya kwamba wakati umewadia. Wakati umefika, ahadi ya Mungu kutimia.

74 Sasa, siku moja, akitembea kwa vishindo kutoka nyikani, alikuja nabii akiwa na Nguzo ya Moto juu ya ninii chake . . . juu yake, ikimwongoza. Alifanya miujiza na kadhalika, na kuwaambia ya kwamba kulikuwa na nchi iliyojaa maziwa na asali. Hakuna mtu aliyewahi kuwa huko, hata mmoja wao, walisikia tu habari zake, “Imani chanzo chake ni kusikia.”

Kwa hiyo wakatoka wakaenda, pamoja na nabii huyu, kupitia nyikani.

75 Ndipo wakafika mahali paitwapo Kadesh-barnea. Hapo wakati mmoja palikuwa ndipo kiti cha hukumu cha ulimwengu. Basi hapo Israeli walipopiga kambi . . . Na hapo ndipo ilipohukumiwa, na dhambi. Naye Yoshua, shujaa mkuu, na neno *Yoshua* linamaanisha "Yehova Mwokozi," shujaa huyu mkuu alivuka Yordani, hakuna hata mmoja wao aliyewahi hapo awali, kuvuka Yordani wakaingia nchi hii ya ahadi, ndipo akarudi na ushahidi kwamba ilikuwa nchi nzuri, na ilikuwa ni kweli.

76 Alikuwa anafanya nini? Akithibitisha Neno la Mungu, mnaona, akionyesha kwamba yale Mungu alikuwa ameahidi, Mungu alikuwa amefanya. Mnaona, hilo agano halina masharti.

77 Mungu alifanya maagano matatu, moja pamoja na Adamu, akalivunja; lingine pamoja na Nuhu, nalo likaninii . . . likavunjwa; lakini Mungu alipofanya agano na Ibrahimu, lilikuwa "Nitafanya," sio, "Kama utafanya," alisema, "Nimefanya," ni agano la Mungu lisilo na masharti ambalo Yeye alifanya pamoja na Ibrahimu na Uzao wake. Nasi tunakuwa Uzao wake wakati tumekufa katika Kristo.

78 Sasa angalieni, na katika wakati huu mkuu, aliporudisha ushahidi, Israeli walihamia humo nchini, na huko haikuwalazimu kuwa chini . . . watumwa. Wangeweza kuwa na bustani zao wenyewe, na kuwalea watoto wao, na kulea makanisa yao, na kadhalika. Lakini hatimaye uzee ukaanza kuwafikia, baada ya muda kidogo kwenye nchi hiyo nzuri ya ahadi yalitapakaa mawe ya makaburi ubavuni mwa vilima kila mahali.

79 Kisha kutoka Utukufuni akashuka aliye mkuu kuliko Mashujaa wote, Yehova Mwokozi mwingine, Yesu, Mwana wa Mungu. Naye akasema kwamba kuna Uhai baada ya mauti, ambako hakuna mawe ya makaburi wala eneo la makaburi, "Kwa maana Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Kama sivyo ningaliwaambia. Nami nitakwenda na kuwaandalia mahali, kisha nirudi tena kuwakaribisha Kwangu."

80 Alikuja kuokoa jamii ya wanadamu inayokufa, Naye akafika Kadesh-barnea Yake, Kalvari, hukumu, ambapo, si kiti cha hukumu cha ulimwengu tu, bali alihukumiwa kwa ajili ya ulimwengu. Hapo aliuchukua uovu na dhambi zetu sote pale Kalvari, naye akafa, mpaka jua na mwezi na nyota hazingeweza kuangaza. Naye akavuka Yordani, tunayoiita Yordani, "mauti." Lakini katika siku hiyo ya tatu akafufuka tena, akirudisha ushahidi kama Yoshua alivyofanya, "Hiyo Nchi ipo. Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai milele hata milele, nami ninazo funguo za mauti na kuzimu." Hajafa, Yeye amefufuka.

81 Basi tuna arabuni ya Urithi wetu, ameliambia Kanisa, "Pandeni mwende kule Pentekoste, hadi kwenye—kwenye . . . siku kumi huko Yerusalemu, ngojeni huko *muda fulani.* Nitawatumia arabuni ya Nchi hii kuu." Nasi tunaungama dhambi zetu, kisha tunakufa kwa nafsi zetu, na tunafufuka pamoja Naye, nasi tunao ushahidi.

82 Angalieni mahali tulipokuwa, angalieni tulipo. Amina. Mnaona, wakati mmoja tulikuwa *huko* chini, sasa tuko *hapa* juu, tayari tumeshikilia ushahidi kwamba tumekufa na kuzikwa ndani ya Kristo, na kufufuka tena katika ufufuo, na kuketi, usiku wa leo, pamoja Naye katika mahali pa mbinguni katika Kristo Yesu. Loo, jamani. Kila ibilisi, kila maradhi, kila ugonjwa, kila kitu kimeshindwa na Yeye. Yeye ndiye mshindi huyo mkuu. Hatuna haja ya kushinda tena, tayari imeshindwa. Tayari tumekufa, tumefufuka tayari, amina, tayari tumefufuka katika wafu.

83 Ni wangapi hapa ndani wanaojisikia hivyo usiku wa leo? Angalieni tu hapa. Tayari tumefufuka katika wafu, wakati mmoja mlikuwa mmekufa katika mashaka, makosa, mkitilia shaka Neno la Mungu, mkatilia shaka kwamba ni la kweli.

84 Sasa, mnasema, "Watu wengine ni wa kidini tu, wanaacha tu wizi, wanaacha uwongo." Hao—hao sio Wakristo, hao ni watu wanaojifanya tu. Sikuzote kuna matabaka matatu ya watu, kila mahali, hao ni waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Mnao katika kila kundi, wapo—wapo kila wakati. Kwa hivyo watu wananinii tu . . . Lakini maungamo, huinuka, wakasema, "Vema, niliungama dini zamani sana." Wenye mashaka. Mnaona?

85 Jambo unalotaka kufanya ni kufa kwa nafsi yako mwenyewe, kisha uzikwe ndani ya Kristo, na kufufuka pamoja Naye katika ufufuo Wake, na kuketi sasa katika mahali pa Mbinguni. Mnaona? Ndipo kutokuamini kwako kunapita.

86 Roho wa Mungu anawezaje kukaa ndani yako, na kulikana Neno, wakati Roho wa Mungu aliliandika Neno? Unaona, huwezi kufanya hivyo. Kama ukilikana Neno, kuna kitu ndani yako kinachokwambia sivyo lilivyo, basi huko ni kutokuamini, ungali katika dhambi. Waangalie wale makuhani na Mafarisayo, jinsi walivyokuwa wa kidini, watu watakatifu, kama ambavyo tungewaita siku hizi, naye Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi, na kazi zake mnazifanya." Nini? Kulitilia shaka Neno. "Mlichukua mapokeo yenu, na kuzitangua amri za Mungu." Loo!

87 Kama angalikuwa hapa usiku wa leo, lingekuwa ni jambo lile lile, mapokeo yetu yamelitangua Neno la Mungu kwa watu. Hatuna budi kurudi kwenye Neno hilo, kulirudia.

88 Samahani, marafiki zangu weusi, ninawahubiria kila mahali, lakini dada mkongwe alitoa ushuhuda si muda mrefu

uliopita katika moja . . . mkutano, akasema, "Mimi taka kutoa ushuhuda."

"Vema, Dada. Endelea."

89 Akasema, "Nataka kusema hivi: mimi siiko ninavyopaswa kuwa, wala siiko ninavyotaka kuwa, lakini kuna jambo moja la hakika kwangu, siiko jinsi nilivyokuwa zamani." Kwa hivyo nafikiri hilo ni wazo zuri. Mnaona? "Si—si—siiko *kule* chini tena, wala mimi si mzuri kadiri ninavyotaka kuwa, wala si mzuri jinsi ninavyopaswa kuwa, lakini nina uhakika wa jambo moja, siko chini *kule* tena." Hiyo ni falsafa nzuri. Naam, bwana. Si—siko nilivyokuwa. Hiyo ni kweli.

90 Sasa, tungeangalia nini katika Kristo basi? Sasa, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, itabidi tujue alivyokuwa jana tupate kujua alicho leo. Je, hiyo ni kweli? Kwa maana, huenda nilisema katika maneno haya yaliyokatikakatika kwamba Yeye ni—Yeye ni yule yule, Biblia ilisema hivyo, nami ninajaribu kuwaambia Mungu asiye na mwisho hawezi kubadilisha njia Yake, Yeye hana budi kubaki vile vile. Kwa hiyo, kile alichokuwa . . .

91 Sasa, hiyo ilikuwa katika siku za Paulo, akiandika Kitabu cha Waebrania hapa, tunaamini kuwa ni Paulo, Naye alikuwa akiwaambia hao Waebrania ya kwamba Yesu Kristo alikuwa yeye yule jana. Sasa, tunajua ya kwamba Yesu Kristo alikuwa Ndiye Yule—Yule aliyewatoa wana wa Israeli kutoka Misri, sote tunaamini hilo. Ile Nguzo ya Moto, ilikuwa ni Kristo, bila shaka ilikuwa. Biblia ilisema katika Waebrania 11 hapa, ninaamini, kwamba "Musa alihesabu kushutumiwa kwake Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri." Mnaona? Alimfuata Kristo, na mtu yeyote anajua ya kwamba ile Nguzo ya Moto, Nuru, iliyowapeleka Israeli kupitia nyikani ilikuwa ni Malaika wa Agano, ambaye alikuwa ni Kristo.

92 Kama mtaelewa, Yeye alikuwa . . . Huyo alikuwa ni Mungu juu yetu, na ndipo, alipofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake, na sasa Yeye yuko ndani ya Kanisa, mnaona, mnaona, "yeye yule jana, leo, na hata milele." Mnaona? Sasa, angalieni kile alichokuwa jana. "Sisi tunataka kumwona Yesu."

93 Sasa, kama tulimwona jinsi alivyokuwa wakati huo . . . Sasa, hebu tuchukue . . . Tunasoma kutoka katika Yohana Mtakatifu, na Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza hapa ilisema, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Basi ni nini? Neno. Kama tulimwona Kristo kama alivyokuwa jana, angekuwa Neno la Mungu, kwa sababu "Hapo mwanzo alikuwako Neno, Neno alikuwa pamoja na Mungu,

naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Sasa, Yeye angekuwa Neno la Mungu.

94 Alipokuwa hapa duniani alikuwa mkamilifu sana juu yake, ameshawishika sana, akasema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa maana ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia." Amina. "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Haikuwa kwamba . . . Hawangeweza kumwelewa Mtu huyu kuwa si zaidi ya mtu wa kawaida tu. Vema, kimwili pengine hakuwa, bali alizaliwa na bikira, lakini hata hivyo, Yeye alikuwa Mwanadamu, alikula, akanywa, akalala, na kadhalika kama sisi tufanyavyo, lakini hata hivyo, ndani Yake mlikuwa na Mungu.

95 Alisema, "Si Mimi nizifanyaye kazi hizo, ni Baba Yangu akaaye ndani Yangu, Yeye huzifanya kazi hizo." Katika Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo Mwana alitendalo vile vile. Sikuzote Mimi hufanya yale yampendezayo Baba." Kwa nini? Hakutenda mpaka aliposikia; Baba alimwonyesha la kufanya. Loo, laiti tungengoja namna hiyo, naam, bwana, mpaka tuone.

96 Mnaona, alisema, "Mwana hatendi neno kwa nafsi Yake," au, "hawezi kutenda neno ila lile amwonalo Baba analitenda." Mwana hutenda kazi- . . . "Baba anatenda kazi, naye Mwana anatenda kazi vile vile." Mnaona? Kwa neno lingine, Yeye aliigiza tu yale Mungu aliyomwambia afanye. Sasa, Yeye angekuwa Neno. Na hilo ni . . .

97 Ninaamini ya kwamba Biblia hii, Neno hili papa hapa, Biblia, ni Mungu katika hali ya maandishi. Nami ninaamini ya kwamba Biblia ni Mbegu, Maneno hayo ni Mbegu. Yesu alisema, "Mpanzi alitoka akaenda kupanda Mbegu." *Hii* ndiyo. Neno la Mungu ni Mbegu, Yesu alisema ndivyo.

98 Basi, kama ni Mungu katika hali ya maandishi, nawe ulipokee moyoni mwako, kisha Roho Mtakatifu aitie maji hiyo Mbegu, itazaa kile alichoahidi. Na aina yoyote ya mbegu unayopanda, itazaa aina hiyo ya zao. Kweli kabisa. Tumepanda, katika uamsho huu mkuu unaopita, mbegu nyingi za kiakili, tuna zao la kiakili. Hiyo ni kweli. Kama tungepanda Mbegu ya Injili, tungepata Zao la Injili. Basi inatupasa kurudi kwenye kanuni, na mafundisho ya Biblia, kurudi kwenye Biblia, kurudi kwenye Roho Mtakatifu juu ya Neno la Mungu ambaye hulihuisha Neno la Mungu. Hivyo ndivyo lilivyokuwa hasa.

99 Sasa, Yeye alikuwa Mwana wa Mungu wakati alipozaliwa. Lakini alipobatizwa na Yohana huko Yordani, walimwona Roho Mtakatifu akishuka kama hua na kukaa juu Yake. Na Yeye akiwa ni Neno, basi Neno likaanza kujionyesha Lenyewe. Amina. Neno likaanza kujidhihirisha Lenyewe. Kwa nini? Roho Mtakatifu alikuwa mle ndani akilinena Neno la Mungu.

100 Sasa, tunaona ya kwamba katika Waebrania, mlango wa 4, kifungu cha 12, Biblia ilisema kwamba "Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, likikata kugawanya," na kadhalika, "na Huyatambua mawazo na makusudi ya moyo," Waebrania 4:12. "Neno . . . " Sasa, msisahau hilo sasa, tutalihitaji baada ya kitambo kidogo. "Neno, Neno la Mungu Huyatambua mawazo ya moyo."

101 Sasa, Kumbukumbu la Torati 18, Musa, yule nabii mkuu, kuhani, na mfalme, chochote alichokuwa, aliyewaongoza Israeli, alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi. Itakuwa kwamba mtu ambaye hatamsikia Nabii huyo atakatiliwa mbali."

102 Mnakumbuka Yohana alipokuja? Ilikuwa ni miaka mia nne tangu wawe na nabii, tangu Malaki. Naye Yohana alipofika alilitikisa eneo hilo. Wakamjia na kusema, "Je, wewe ndiye yule Nabii," mnaona, "aliyepaswa kuja?"

Akasema, "Mimi siye. Lakini anakuja nyuma yangu."

103 Sasa, Yohana alikuwa tu akihubiri. Mnaona? Alikuwa nabii, lakini m—mhubiri wa Neno ni nabii. Lakini Israeli daima walifundishwa kuamini manabii wao, kwa maana Neno la Bwana humjia, nani? Nabii. Hiyo ni kweli. "Neno la Bwana lilimjia nabii Isaya." "Neno la Bwana lilimjia nabii Yeremia." Neno la Bwana liliwajia manabii.

104 Waebrania 1, "Mungu, alisema zamani na baba zetu kwa njia mbalimbali. Siku hii ya mwisho, kupitia Mwanawe, Kristo Yesu." Angalieni, Waliwajia manabii, nao Israeli walifundishwa kuamini manabii wao.

105 Wengi wenu mnamfahamu Lewi Pethrus, rafiki msiri wangu sana, alituma takriban Agano Jipya milioni moja kule chini, walipowaleta wale Wayahudi kutoka huko chini Iran, wakiwapa hizi Agano Jipya. Mnajua Agano la Kiyahudi, unasoma kuanzia nyuma kwenda mbele, na hawa Wayahudi wakilisoma Hili, hawakuwahi kusikia juu ya kitu kama Yesu kuwa Masihi.

106 Walikuwa wamechukuliwa kule chini katika utumwa wa Kirumi. Wangelima kwa . . . Mliliona katika gazeti la *Look* hapa, miaka michache iliyopita, na wakati waliporudi. Nami nina picha yake, wote wakirudi ndani. Laiti tungalikuwa na wakati tungeirusha kwenye skrini usiku fulani, na kuwaonyesha. Wanaiita . . . Tunaiita *Dakika Tatu Ifike Usiku Wa Manane*, kuwaona hawa Wayahudi wakirudi, wakiwabeba wapendwa wao migongoni mwao, wakishuka kwenye ndege, na kadhalika. Wanasema . . . Walisema, "Je, mnakuja nyumbani, kwenye nchi ya wenyeji, mpate kufa?"

Akasema, "Tunakuja kumwona Masihi."

107 Hmm, jamani! "Wakati mtini utakapotoa machipukizi yake!" Hilo hapo, taifa lenye pesa zake na kila kitu kingine,

sarafu, jeshi lake lenyewe, na kila kitu, mara ya kwanza kwa miaka elfu mbili mia tano. Mnaona? Yesu alisema, "Mtakapouona ukitoa machipukizi . . . " Sasa tuko kwenye wakati wa mwisho.

108 Angalieni. Sasa, walikuwa . . . Walipoenda kupanda ndege hizo, hawakutaka, waliogopa ndege hizo. Kwa hiyo rabi akawaita na kusema, "Kumbukeni, nabii wetu alisema tutapelekwa nyumbani kwa mbawa za tai." Ndiyo hiyo, ndege. Kwa hivyo wakapanda. Nao hao hapo, wameketi katika nchi ya wenyeji wao. Wanaamini manabii wao.

109 Sasa, kwa hiyo, wakati ilipompasa Masihi kuja Yeye alipaswa kuwa Nabii-Mungu. Alipaswa kuwa Nabii na zaidi, zaidi ya nabii, lakini alipaswa kufanya kazi za nabii.

110 Lewi Pethrus, alipotuma Biblia hizo kule chini . . . Alisema, "Ikiwa huyu Yesu alikuwa ndiye Masihi, basi hajafa, mnasema, bali amefufuka tena, hebu tumwone akifanya ishara ya nabii, nasi tutaamini hilo." Loo jamani, hilo litakapotukia, Mataifa wamekwisha, nanyi mwajua hilo. Ninyi nyote wasomaji wa Biblia mnajua hilo. Huo ndio wakati wa mwisho hapo wakati . . . Hebu hao Wayahudi walipate tu tena, basi . . . Jambo kamili tu kwa muda kidogo tu wa kupumzika sasa. Wakati milango ingali wazi, Mungu anayo—Mataifa wakiwapokea hao wengine wanaoingia, watakaokuja, milango ya rehema.

111 Sasa, hebu tuone kile Yeye alichokuwa. Tunamwona basi akiwa Neno, alibatizwa, akaenda nyikani, akatoka baada ya kujaribiwa siku arobaini, ibilisi. Na mara Yeye—Yeye akaanza . . . Sifa Zake zikaanza kuenea. Hata hivyo, Yeye . . . Nadhani hakuwa m—mhudumu ambaye angekuwa . . . sikia Sauti Yake kama yetu barabarani, na kadhalika, bali kulikuwa na jambo kumhusu ambalo lilikuwa ni tofauti.

112 Nasi tunaona, mara tu alipoanza huduma Yake, kulikuwa na mtu jina lake Andrea, Yohana Mtakatifu hapa, moja . . . Ninakaa papa hapa katika Yohana Mtakatifu kwa muhtasari wangu uliobaki kwa sasa hivi. Mtu mmoja, jina lake Andrea, alikaa na Yeye usiku kucha, naye akashawishika kabisa kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, akamwendea Simoni. Sasa, ikiwa yeyote- . . . Huyo ni kaka yake.

113 Ikiwa mtu yeyote aliwahi kusoma historia ya Petro na—na Andrea, kama tunavyowajua, baba yao alikuwa mwaminio hodari, aliwaambia hao wavulana, "Siku moja . . . Si—sikuzote nimewazia ningemwona Masihi." Kila Myahudi ametamani jambo hilo tangu Edeni. Na hivyo wakasema, "Tumeninii . . . Sisi . . . Siku moja Masihi atakuja. Nilidhani nisingeninii . . . kumwona, lakini labda ninazeeka wala sitamwona. Lakini, enyi wavulana, kabla tu ya huyo Masihi ajaye, kumbukeni, kutakuwako na mambo mengi sana yatakayotokea."

114 Daima kuna masihi wanaokuja, tunajua hilo, kila mahali, tungali tunao kila mahali, masihi. Vema, kama masihi wote wa uongo wakija, inaonyesha lazima kuwe na Masihi wa kweli mahali fulani. Kabla hapajaweza kuwa na dola ya bandia, lazima kuwe na nzuri ili itengenezwe kutoka kwake, hiyo ndiyo sababu ni ya bandia.

115 Angalieni, aliwaambia wanawe, akasema, "Sasa, msisahau, dumuni na Maandiko. Masihi, kulingana na Musa, yule ambaye tulimfuata miaka hii yote, alisema, 'Bwana Mungu wetu atainua Nabii miongoni mwetu.' Atakuwa nabii, Masihi hatakuwa tu mwanachuoni, mwelimishaji, kuhani fulani mkuu, mtu fulani mashuhuri, lakini Yeye atakuwa nabii." Sasa, tutamtafuta sasa, kwa kama dakika kumi tu sasa, kabla hatujaanza kuwaombea wagonjwa. "Atakuwa ni nabii."

116 Basi Andrea anaenda na kumwona Simoni, ndugu yake mvuvi, naye akasema, "Njoo, umwone Yule tuliyemwona. Tumemwona Masihi!"

Ninaweza kuwazia Simoni akisema, "Loo, naam. Uh-huh. Tumekuwa nao kila mahali."

117 Lakini akaja akitembea Mbele za Yesu, na mara Yesu alipomwona akija, alisema, "Kuwa . . . " alinena naye na kusema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona."

118 Hilo likashika. Alijua papo hapo. Sio tu kwamba Yeye alijua yeye alikuwa ni nani, bali alimjua yule baba yake mzee mtauwa, "Wewe ni Simoni, mwana wa Yona." Papo hapo, kwa Petro huyo alikuwa ndiye huyu Masihi, kwa maana Yeye alikuwa amethibitisha hasa jinsi Maandiko yalivyosema Yeye angekuwa.

119 Si kwa sababu alikuwa amevalia vizuri, alikuwa na digrii *nyingi sana* kutoka chuoni, alizungumza Maneno Yake kwa heshima, alikuwa na ushawishi mkubwa miongoni mwa watu, huyo asingekuwa nabii. Manabii wanachukiwa sana, na kwa hiyo . . . Watu hawawapendi. Ufunuo 11 ilisema wakati hao wawili . . . Mataifa yaliwachukia manabii hao, daima wamefanya hivyo.

120 Yesu alisema, "Ninyi ndio mliowapiga mawe manabii, kisha mkayapaka makaburi yao chokaa," kasema, "Ninyi ndinyi mliowaweka mle. Ni yupi kati ya manabii waliotumwa na Mungu ambaye hamkumpiga mawe?" Daima wao ni kinyume na dhidi ya mifumo ya kidini ya siku hizo. Nasi tunaona ya kwamba wanasimama kwa ujasiri, na huyu hapa Yesu alikuwa amesimama pale nje. Nao waliona, hata hivyo, ya kwamba Yeye alikuwa akifanya ishara ya nabii, ndipo Simoni akasema . . . akamkiri kuwa Mwana wa Mungu.

121 Kulikuwa na mmoja aliyesimama pale, jina lake Filipo, papa hapa mistari michache tu chini yake hapa, Filipo, naye alikuwa na mwenzake. Kama uliwahi kuchunguza maisha ya Filipo, alikuwa na mwenzake, ambaye waliketi na kusoma Biblia

pamoja. Tunafanya hivyo mara nyingi sana, tunaketi na kusoma mambo mbalimbali. Nao wahudumu, na ndugu, na walei, na wote husoma Biblia, tunachukua Biblia yetu nyumbani. Marafiki wa kiume, na marafiki wa kike, wanapokuwa Wakristo, na mume na mke, tuna masomo madogo ya Biblia.

122 Nathanaeli na Filipo walikuwa wakisoma Magombo pamoja, nao walikuwa wameshawishika, kwa sababu wote wawili walikuwa waaminio, kwamba Masihi alikuwa . . . wakati wa kuja Kwake ulikuwa umewadia. Kwa hiyo Filipo alipoona hilo likitukia, alizunguka mlima kumtafuta Nathanaeli.

123 Sasa, kama utaitia alama, kama utawahi kuwa huko, kutoka mahali ambapo Yesu alikuwa akihubiri hadi pale alipomwona Nathanaeli, kwenye kijisitu hicho, palikuwa kama maili kumi na tano. Pengine alikwenda siku moja akarudi kesho yake. Naye akamkuta Nathanaeli, tunajua hadithi hiyo, alikuwa nje katika shamba lake la matunda akiomba, na chini ya mitini akiomba.

124 Nami ninaweza kuwazia nikimwona Nathan- . . . Filipo, akiwa amesimama pale akingoja mpaka alipomaliza kuomba. Na labda alikuwa akiomba namna hii, "Ee Bwana, tuko tayari kwa ajili ya Mkombozi. Bwana, tumekuwa katika utumwa wa Warumi wakati huu wote, watu Wako wanateseka. Ee Mungu, wako . . . wote wamepotea, na inaonekana kana kwamba makanisa yote yameachilia. Tunaomba, Ee Bwana, ututumie Mkombozi, ututumie Masihi, tumemtazamia. Tuliomba na hizi hapa si—siku zinapita sasa kwangu, nami nilitaka kumwona Masihi. Amina."

125 Aliposimama, Filipo akasema, "Njoo, uone Mtu tuliyemwona." Sio, "Mnaendeleaje? Kuku wanaendeleaje, na mayai yako sawa? Na ng'ombe wa maziwa wakoje?" Hapana, hapana. "Bustani ya mizeituni ikoje?" La, moja kwa moja. Hiyo ndiyo shida siku hizi, tuna upuuzi mwingi sana uliochanganyikana na Ukristo. Moja kwa moja kwenye hoja, "Njoo umwone Yule tuliyempata, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu." Hiyo ndiyo njia ya kuusambaza ujumbe.

126 Sasa, hebu *tuliigize* kidogo kwa ajili ya watoto. Ninaweza kumwazia Nathanaeli, msomi wa Maandiko, mwajua, akisimama, kasema, "Sasa, Filipo, mimi na wewe tumejifunza Maandiko kwa miaka mingi, tangu tulipokuwa wavulana kutoka shuleni. Nawe hapana shaka uliingia wazimu mahali fulani," kama ambavyo tungesema siku hizi. "Unamaanisha nini, msomi kama wewe katika Maandiko? Na—nawe ungesema ati, 'Tulimwona Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu, akiwa Masihi'? Mbona, haiwezekani, hakuna kitu chochote chema kinachoweza kutoka huko."

127 Sasa, yeye . . . Nafikiri alimpa jibu zuri sana, hakusema, "Kaa nyumbani ukakosoe." Alisema, "Njoo ujionee mwenyewe." Mnaona? Njoo ujionee mwenyewe. "Njoo uone."

128 Ninaweza kuwazia wakienda zao barabarani kesho yake. Mbona, ninaweza kumsikia Nathanaeli akisema, ama, Filipo akimwambia Nathanaeli, "Unajua nini? Hivi unamkumbuka yule mvuvi asiye na elimu . . . ?"

129 Sasa, mnamkumbuka, Petro, askofu, uongozi wa kanisa la kwanza, hakuwa na elimu ya kutosha kusaini jina lake mwenyewe. Biblia ilisema alikuwa asiye na elimu wala maarifa. Lakini ilimpendeza Mungu, kwa imani yake, kumtambua Yeye alikuwa ni Nani. Mnaona? Hata alimpa funguo za Ufalme . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . bila elimu ya kutosha kusaini jina lake.

Naweza kumsikia akisema, "Je, unamkumbuka yule mvuvi mzee ambaye ulinunua yule samaki kutoka kwake wakati ule?"

130 "Loo, naam, wa—wanamwita Simoni. Naam, nakumbuka, nilimjua baba yake, Yona. Hakika. Alikuwa Farisayo mzee kule juu, shemasi kanisani, mwajua," na kadhalika.

"Naam."

"Unakumbuka, uliwanunua wale samaki, naye hakuweza kutia sahihi risiti ile."

"Naam."

131 "Alikuja mbele za jamaa huyu, Yesu, huyu Nabii kijana wa Galilaya, Naye akamwambia jina lake lilikuwa nani, na kumwambia baba yake alikuwa nani. Unakumbuka jinsi . . . ? Mbona, haitanishangaza kama Yeye hataniambia ni nani . . . akwambie wewe ni nani ukifika huko."

"Loo, laiti ningeweza kuona hilo!"

132 "Sasa, tunajua ya kwamba sote tulisoma Maandiko. Tunakubaliana kwamba Musa, hatuna budi kuchukua neno lake, kwa sababu alikuwa kibao kikuu cha kutangazia cha Mungu, naye alisema ajapo Masihi Yeye angekuwa nabii. Sasa, inatubidi tu kukumbuka Yeye ni nabii."

Naye akasema, "Loo, naam. Hakika, Masihi ni nabii."

"Vema, Mtu huyo alijuaje Simoni alikuwa nani, ama baba yake alikuwa nani? Baba yake amekufa miaka mingi."

Sasa, alisema, "Naam, nitaenda tu kuona."

133 Ndipo alipoingia ndani . . . Vema, labda Yesu alikuwa akifanyiza mstari wa maombi, ama labda alipanda akaketi kwenye kusanyiko, ama chochote kile. Mimi . . . Baada ya kitambo kidogo, Yesu aligeuka, akamwangalia, akasema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake!"

Sasa, unasema, "Naam, bila shaka, jinsi alivyokuwa amevalia . . . "

134 La, la. Wamisri, wote walikuwa na ndevu, na kadhalika. "Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!" Hakumwita Mmisri, Alisema, "Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!"

Angeweza kuwa mwuaji, ama katili, chochote kile. Mnaona? Lakini alisema, "Huyo hapo Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!" Hilo lilimshangaza kweli.

Akasema, "Rabi," ambalo linamaanisha "mwalimu," "ulinijua lini Wewe? Sijawahi kukuona kabla."

135 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona." Ndilo hilo. Huyo alikuwa ni Yesu jana, miongoni mwa Wayahudi. Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nalikuona."

136 Sikilizeni, labda askofu alikuwa amesimama pale, nijuavyo mimi, lakini upesi-...hilo halikuleta tofauti yoyote kwa Nathanaeli, alikimbia, akaanguka karibu Naye, na kusema, "Rabi, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli." Amina.

Sasa, huyo alikuwa ni Yesu jana? Hivyo ndivyo alivyokuwa akijitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi?

137 Sasa, kulikuwa na wale wanachuoni mashuhuri, wakuu, wamesimama pale wakiwa wamevaa vilemba vikubwa, ukosi uliopinduliwa, mwajua, na kadhalika. Wakasema...Vema, iliwabidi kutoa jibu kwa kusanyiko lao, hapo lilitendeka, kwa hiyo wakasema, "Mtu huyu ni Beelzebuli." Huyo ni ibilisi, mpiga ramli. Mnaona? Naye akasema, "Anafanya hivyo kwa Beelzebuli, ibilisi."

138 Naye Yesu akasema, "Nimewasamehe hilo. Lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja kufanya jambo lile lile, na kusema neno moja dhidi yake hamtasamehewa kamwe." Hiyo ni kweli.

139 Sasa, kuna ninii tatu...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...jamii za watu. Huenda msitake kuamini, lakini zipo. Ikiwa tunaamini Biblia, wote walitoka kwa Hamu, Shemu, na Yafethi, watoto wa Nuhu.

140 Sasa, angalieni, Petro alipokuwa na funguo za Ufalme, aliruhusu...alihubiri huko Pentekoste, Wayahudi, wakampokea Roho Mtakatifu, na wale waliokuwa pale, kisha Filipo akashuka na kuwahubiria Wasamaria, ila tu walikuwa bado hawajampokea Roho Mtakatifu, ndipo Petro akashuka, akawawekea mikono, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Na halafu, kwenye nyumba ya Kornelio, Mataifa, Petro alipanda kule, naye alitumwa kwa ono kule juu, "Basi alipokuwa angali anazungumza, Roho Mtakatifu akawashukia." Na ndipo jamii zote zikampokea, mnaona, zile jamii tatu, hao walikuwa ni Wayahudi, Mataifa, na Wasamaria.

141 Sasa, Mmataifa, sisi, Anglo-Saksoni, hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote, tulikuwa tukiabudu sanamu, rungu mgongoni mwetu, na ni wapagani, lakini...katika watu wetu. Lakini Masihi huja tu na kujitambulisha kwa wale wanaomtazamia Masihi. Yeye kamwe hajisukumizi kwa mtu

yeyote; huna budi kumwonea shauku. Na kwa hiyo akasema . . . Alikuja . . . Sasa, tutalichukua baadaye kidogo, kwa maana hatutaki wakati wetu umalizike, tumebakisha dakika chache tu.

142 Angalieni, wakati alipokuja, alijitambulisha kwa Wayahudi kwa kuwa ni Masihi, kwa kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye yule Nabii ambaye Musa alimwinua, au, aliyenenwa na Musa, hasa, ya kwamba alikuwa ndiye Masihi, kwa sababu alifanya ishara ya Masihi. Nao walijua huyo alikuwa ndiye Masihi. Aliyatambua mawazo yao, hilo ni Neno, "kali kuliko upanga ukatao kuwili, Huyatambua mawazo ya moyo." Hiyo ni kweli? Naye alikuwa Neno, naye Huyu hapa, akitambua wazo lao.

143 Ndipo siku moja alikuwa akishuka kwenda Yeriko, huko ni moja kwa moja kutoka Yerusalemu. Badala ya kwenda huko, alikuwa na haja, kupitia Samaria. Angalieni, Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi pia. Basi akafika mji uitwao Sikari, akawatuma wanafunzi waende kununua chakula, nao wakiisha kuondoka, maskini mwanamke mmoja akaja pale, labda msichana mrembo. Labda huyo mtoto aliachiliwa mtaani na wazazi, na kumwacha aende kwa njia yoyote, na ni kama siku hizi.

144 Wanazungumza juu ya kutowajibika kwa vijana, ni kutowajibika kwa wazazi, ndivyo ilivyo hasa. Labda mtoto huyo alikuwa na jambo lile lile, mama alimwachilia afanye lolote. Aligeuka kuwa mwanamke mwenye sifa mbaya. Wala hakuweza kutoka . . .

145 Sasa, nimekuwa katika nchi za mashariki, na kuhubiri huko kwa . . . vema, kusanyiko kubwa zaidi nililopata kuwa nalo lilikuwa ni laki tano, hilo lilikuwa huko Bombay, kule, mnaona. Na—na huko . . . Nami na—na—najua desturi zao. Sasa, wasio waadilifu na walio waadilifu hawawezi kushirikiana pamoja. Hivyo mwanamwali . . . Vema, hakuna hata mmoja wao angeweza kuja kule wakati wanawali walipokuwa pale, kwa hiyo ilimbidi atoke baadaye. Yapata saa tano akatoka, labda nywele zake zilikuwa zimesukwa juu ya kichwa chake, na—naye alikuwa . . . labda alikuwa ametoka usiku kucha pia, mwajua, naye akaja kuchota ndoo ya maji.

146 Nazo ndoo zao ni vyungu, vina tambo. Na wanaweza kuweka ninii . . . Inaonekana kwangu kama vinaenea takriban galoni tatu hadi tano. Wanaweza kuweka moja ya vyungu hivyo juu ya kichwa chao, na kuweka moja kwenye kila nyonga, na kutembea na kuzungumziana, kama tu vile wanawake wawezavyo, na kamwe wasimwage hata tone la maji. Sijui jinsi wafanyavyo hilo, wanaendelea tu mbele, wakizungumza mwajua na kucheka, maskini wasichana hao, si warefu *hivi*, wakivibeba tu, takriban galoni kumi na tano za maji, wakienda zao.

147 Na kwa hiyo wa—wana winchi huko, nao wanachukua hivi viopoo na kuvizungushia tambo hizi, wanaachilia . . . kama mtungi, tungeuita, wanauachilia kisimani na kuchota maji, na kisha wanauinua kwa hiyo winchi.

148 Ndipo, mwanamke huyu akaja huko ku—kuitelemsha ndoo yake ateke maji, na alipofanya hivyo, akamsikia Mwanamume ameketi kwenye namna fulani ya mandhari hivi, ni kisima, bado kipo, akasema, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

149 Naye akatazama, na kulikuwa na ubaguzi nchini kati ya Wayahudi na Ma- . . . , au, Wayahudi na Msamaria. Kwa hiyo wakasema . . . mwanamke huyu akasema, "Bwana, si kawaida Kwako, ukiwa ni Myahudi, kuniomba mimi, mwanamke Msamaria, kitu kama hicho."

150 Sasa, Yeye alionekana tu kama Myahudi wa kawaida, alivalia kama mtu wa kawaida. Siamini kwamba inakubidi kuvalia kiajabuajabu na kuwa tofauti upate kuwa Mkristo, siamini kwamba unapaswa kutenda kiajabuajabu. Ninaamini u—uwe tu mtu, kuwa tu Mkristo, hivyo tu, na hakuna kitu cha kipekee. Ni jambo fulani tu ndani yako linalopaswa kutukia, unaona, furaha, shangwe, na amani, na utoshelevu, uvumilivu, upole, amani; watu wanaweza kuongea juu yako, halikusumbui hata kidogo, unaona, ninii tu, hayo ni matunda ya Roho.

151 Kwa hiyo basi Mtu huyu alikuwa ameketi pale, amevaa joho dogo, kama tu hao wengine walivyokuwa, na kuvalia tu kama mtu wa kawaida. Lakini Yeye alikuwa na takriban umri wa miaka thelathini, lakini hapana shaka alionekana kuwa mzee zaidi, mwajua, katika Yohana Mtakatifu 6, walisema, "Unataka kuniambia kwamba ulimwona Ibrahimu, nawe hujapata bado umri wa miaka hamsini?" Mnaona, walimwona kama mwenye hamsini hivi, huenda kazi Yake ilisababisha hilo.

152 Naye akasema, "Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Kwa hiyo hilo liliyakata manyoya tena, mwajua. Lakini hapo alionekana yuna kama umri wa miaka hamsini, huku ameketi ameegemea nyuma hapo, na kusema . . .

"Mbona," akasema, "si kawaida kwenu Wayahudi kutuomba sisi Wasamaria mambo kama hayo. Hatuna uhusiano sisi kwa sisi."

Akasema, "Lakini kama ungalijua ni Nani unayezungumza naye, ungeniomba Mimi maji unywe."

153 Nanyi mwajua, basi walifanya maho- . . . akachanganyikiwa hapo, mwajua, kuhusu mahali alipoabudia. Sasa, mwangalie mwanamke huyu. Alisema, "Bwana," akasema, "baba yetu Yakobo," sasa, mnaona, huyo alikuwa ni baba wa Wayahudi pia, "baba yetu Yakobo ndiye aliyechimba kisima hiki, yeye na mifugo wake wakanywea humo." Naye kwa kweli akakikabidhi kwa Yusufu, kile alichofanya. Lakini kasema—kasema, "Hiki ni . . . Baba zetu walikinywea kisima hiki. Nawe unasema ati una

Maji ambayo ni bora kuliko haya?" na kadhalika. Halafu baada ya muda kidogo . . .

154 Anajaribu kufanya nini? Alikuwa akiwasiliana na roho yake, kwa maana Neno la Mungu ni nini? "Huyatambua," hebu tuseme, "Huyatambua mawazo ya niani." Mnaona? Anafanya nini? Alikuwa akiongea naye, akiwasiliana na roho yake, ndipo akapata shida yake. Ni wangapi wanaojua ilikuwa ni nini? Hakika, sote tunajua, Yeye akasema, "Nenda, kamwite mume wako mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume yeyote."

Akasema, "Umesema vema, kwa kuwa umekuwa na waume watano, naye unayeishi naye sasa siye mume wako. Umesema vema."

155 Mwangalie mwanamke huyo. Waangalie Mafarisayo hawa, na waliofunzwa *juu-na-juu*. Mnaona? Walisema, "Mtu huyu ni Beelzebuli. Yeye ni ibilisi." Angalia wakati Nuru hiyo ilipomulika kwenye maskini Mbegu hiyo pale iliyochaguliwa tangu zamani, ilipoigusa ile Mbegu halisi ya Mungu iliyokuwako, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, pengine, jina liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, wakati ilipoigusa Hiyo, upesi akaitambua. Katika hali yake, aliitambua. Ndugu, ninasema mwanamke huyo alijua mengi zaidi kuhusu Mungu wakati huo, kuliko nusu ya watu nchini Marekani. Kweli. Naam, alitambu-. . . Kwa nini? Alichaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mnaona? Wakati Nuru hiyo ilipoigusa . . .

156 Hao Mafarisayo, walikuwa na elimu, na walikuwa na theolojia nyingi sana na kadhalika, bali hawakujua Neno. Na kusema . . . Alisema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii." Whiu! Ni tofauti jinsi gani kati ya huyo, na kuhani huyo mkuu na hao wote, mwajua. "Naona kuwa Wewe ni nabii. Tunajua, sisi Wasamaria, tunajua ajapo Masihi, hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake." Loo, jamani. Myahudi, sasa Msamaria. "Tunajua ajapo Masihi atatwambia mambo haya."

157 Akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye." Huyo alikuwa ni Yesu jana. Mnaona kile alichokuwa? Si mavazi Yake tofauti, si sura Yake tofauti, si chochote Chake tofauti. Alikuwa . . . Kile kilichokuwa ndani Yake, kikimdhihirisha! Haleluya! Huh. Nilianza kusema, "Samahani," lakini nisingeweza kusema hivyo, ningekuwa mwenye kukufuru. Na—naweza nikatenda kiwazimu kidogo, lakini ninajisikia vizuri hivi. Kwa hiyo achana tu na mimi, mwajua. Ninajisikia vizuri zaidi hivi.

158 Angalieni, aliposema, "Hapana shaka wewe ni nabii." Alijua hawakuwa wamekuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Kasema, "Hapana shaka wewe ni nabii. Tunajua ajapo Masihi, tumefundishwa hivyo, tunajua kwa Maandiko, ya kwamba ajapo

Masihi Yeye atatwambia mambo haya, hayo yatakuwa ndiyo mambo atakayofanya."

Yesu akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

159 Na kutokana na hayo akaacha mtungi wake wa maji akakimbilia mjini. Sikilizeni ujumbe wake sasa. Sasa, kumbukeni huko mashariki, ni vile vile tu hasa, hawatamsikiliza mwanamke mwenye sifa mbaya, lakini . . . huyo mtu mitaani, lakini usingeweza kumzuia, ameishapata kitu fulani. Akakimbilia mjini, ilibidi wamsikilize, kama nyumba inayowaka moto, iliwabidi kumsikiliza. Alikimbia mjini na kusema, "Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?" Nayo Biblia ilisema ya kwamba watu wa mji huo walimwamini, kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke huyo.

160 Huyo alikuwa ni Yesu jana. Je, hiyo ni kweli? Ni yeye yule leo. Je, tuna muda wa tamshi moja zaidi? Ninii tu . . . Na kisha ni—nitaanzisha mstari wa maombi, jambo moja tu sasa. Sasa, kumbukeni, jinsi anavyojithibitisha Mwenyewe mwishoni mwa kila wakati, hana budi kulifanya kila wakati. Sasa, huko kulikuwa ni kumalizia kwa wakati wa Kiyahudi, uzao wa kawaida wa Ibrahimu, tunajua, ambao ulitokana na Isaka. Lakini sasa, kuna Uzao wa Kifalme, uliokuja kupitia kwa Kristo, hilo ni Kanisa. Mnaamini hilo? Sisi sote hufanya, hivyo. Sasa, angalieni. Hivyo ndivyo alivyojionyesha Mwenyewe wakati alipowafungia Wayahudi na Wasamaria, katika wakati huo.

161 Angalieni. Sasa, Yesu alisema, katika Luka Mtakatifu, ya kwamba "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." "Kama ilivyokuwa . . . " Sasa, angalia unabii Wake.

162 Sasa, hebu tuone, hebu tuone ni siku ya namna gani Lutu alikuwa nayo. Sasa, kulikuwako na asiyeamini wenu, Wasodoma; Mkristo vuguvugu, wa kimadhehebu, Lutu; na Ibrahimu, Kanisa teule, lililoitwa litoke. Yeye hakuwa Sodoma, walikuwa wametoka Sodoma, kwanza kabisa hawakuwa Sodoma. Kwa hivyo walikuwa na hali mbaya kidogo, lakini wao—walikuwa wangali nje ya Sodoma, hilo ni jambo moja jema.

163 Kwa hiyo Ibrahimu alikuwa ameketi mlangoni pa hema lake, asubuhi moja yenye joto kali, labda yapata saa tano, ndipo Watu watatu wakaja wakitembea, mavumbi nguoni Mwao, Watu tu wakaja wakitembea, Ibrahimu akaangalia. Mwajua, kuna kitu kuhusu hilo. Unaweza, wewe . . . Sijui. A—alijua kulikuwa na jambo lisilo kawaida kuhusu Jamaa hao. Basi akatoka mbio na kusema, "Bwana wangu, njoni huku. Acha nichukue maji kidogo, mkanawe miguu Yenu, ki—kisha niwape chakula kidogo. Halafu basi mnaweza kuendelea na safari Yenu."

Naye akaenda hima ndani, akamwambia Sara aandae mkate. Akatoka nje na kuchukua ndama mdogo aliyenona, akamchinja, kisha akamtoa nje, na kuwalisha.

164 Je, mliona? Wawili kati ya Watu hao, walikuwa kweli . . . Jambo ni kwamba, ilikuwa ni Mungu Mwenyezi. Hiyo ni kweli. Sasa, Biblia hapa, Ibrahimu alimwita katika Mwanzo 18 hapa, 18, alimwita, "Elohimu." Hilo ndilo Jina lile lile ambalo Mungu alionekana ndani yake katika Mwanzo 1, "Yeye Ajitoshelezaye kwa Yote," mnaona, Elohimu, Elohimu, katika mwili. Mnaona?

165 Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, ndugu mhudumu, akasema, "Kweli huamini Huyo alikuwa ni Mungu?"

Nikasema, "Hakika, ninaamini, Ibrahimu alisema alikuwa hivyo, nami ninaiamini Biblia."

Akasema, "Sasa, Mungu angewezaje kuwa katika mwili huo, akila hiyo . . . na kula nyama na vitu kama hivyo?"

166 Nikasema, "Unasahau tu Yeye ni Nani. Sasa, alitaka kuipeleleza Sodoma, kwa hiyo Yeye—Yeye alininii tu . . . " Mwili wa mwanadamu umefanywa kwa takriban elementi kumi na sita mbalimbali, mnajua. Hizo ni, nafikiri ni kwa potashi, na petroli, na nuru-limwengu na kadhalika. Alinyakua tu konzi lake, na "Whiu," akaingia humo ndani, kisha akapulizia konzi nyingine kwa ajili ya Gabrieli, na moja kwa ajili ya huyo mwingine, wakashuka chini. Hivyo tu. Ninafurahi kumjua jinsi hiyo. Nanyi je? Naam, bwana. Anaweza kufanya jambo lolote litumikie kusudi Lake. Kwa hiyo akashuka, hiyo ni kweli, akatoka humo.

167 Nimefurahi sana kwamba siku moja kunaweza kusiwe na hata . . . Nina kama nywele mbili ama tatu zilizosalia, nami nilikuwa nikizichanua hapa si muda mrefu uliopita, ndipo mke akaniambia, akasema, "Billy, umeingia upara kabisa."

Nikasema, "Lakini sijapoteza hata mmoja wazo, mpenzi."

Akasema, "Naomba uniambie, mahali zilipo."

Nikasema, "Sawa, mpenzi, hebu niambie zilikokuwa kabla sijazipata. Popote pale zilipokuwa wakati huo, zinaningoja niziendee."

168 Yeye alisema, "Hata unywele mmoja wa kichwa chako haungeninii . . . " Kweli! Huyo ndiye Mungu wetu. Haijalishi, nimerudi kwenye nurulimwengu, na chochote niwezacho kuwa, Yeye atanena nami nitatoka siku hiyo kwa sababu ninamwamini. Amina. Hiyo ni kweli. Ufufuo. Atanifufua siku ya mwisho, alisema hutapoteza chochote, "Nitakifufua tena, siku za mwisho." Hakika.

169 Huyo hapo, Huyo ndiye Mungu wetu tunayemwamini, Huyo ndiye Mungu ninayenena habari zake. Naye huyu hapa ameketi hapa. Pia angalieni, Wasodoma, wamakanisa, na Kanisa teule. Angalieni. Wawili wao, Billy Graham wa kisasa, na kadhalika, wanashuka kwenda Sodoma, na kuanza kuihubiri Injili, hakuna

mwujiza, lakini kupofusha tu. Na kuhubiri Neno humpofusha asiyeamini. Kwa hiyo akashuka na kuihubiri Injili kuliita kanisa hilo vuguvugu litoke, mnaona, kwa maana uharibifu ulikuwa unakuja, Moto, kinachofuata ni Moto. Lakini Malaika mmoja alibaki nyuma na Ibrahimu. Je, mliona?

170 Hebu tushuke kupitia kwenye wakati tangu wakati huo. Niambie ni lini mlipata kumwona mtu akiingia Babeli . . . Sasa, Ibrahimu alipokea ishara hiyo, na hebu waangalieni hao Malaika walioshuka kule, na siku hizi yule mjumbe kwa kanisa vuguvugu, kanisa la kimadhehebu, linaandikwa, si A-b-e-r-h-a-m, bali G-r-a-h-a-m. Tumekuwa na akina Sankey, Finney, Knox, Calvin, na kadhalika, lakini hakuna moja lililoishia na h-a-m kwa kanisa hilo. Mnaona?

171 Sasa, kuna Malaika aliyebaki nyuma kuonyesha utambulisho Wake, ambaye alikuwa ni Mungu Mwenyewe katika mwili wa mwanadamu, akaonyesha vitambulisho Vyake hapa, akasema, "Ibrahimu," sasa, siku chache tu kabla ya hapo alikuwa Abramu, na kusema, "yuko wapi S-a-r-a, mkeo?" Ambapo, siku moja ama mbili tu kabla ya hapo, alikuwa S-a-r-a-i. "Yuko wapi Sara, mkeo?"

172 Na sasa, huyo Malaika alisema, "Yuko," au, Ibrahimu alisema, "Yuko hemani nyuma Yako." Sasa, wanawake walitenda tofauti kidogo wakati huo, wanavyofanya sasa, mnaona. Hivyo wao . . . Alikuwa hemani nyuma Yake.

173 Kwa hiyo akasema, "Mimi nitakurudia kulingana na wakati wa uhai." Sasa, tazama, "Mimi," kile kiwakilishi nafsi tena, mnaona. Mnaona alikuwa ni Nani? Alikuwa ametoa ahadi, "Nitakurudia kulingana na wakati wa uhai, nawe utampata mtoto huyu wa ahadi," na kadhalika. Naye Sara, ndani ya hema, akacheka kifichifichi. Akasema . . .

174 Sasa, alikuwa mkongwe, umri mkubwa . . . Ninyi ni ninii wangu . . . Nyinyi humsikiliza daktari wenu, mimi ni ndugu yenu. Uhusiano wao wa kifamilia labda ulikuwa miaka kumi na tano, ishirini. Mnaona? Kasema, "Mimi, mwanamke mkongwe, ati ni—nipate raha na mume wangu, naye ni mkongwe pia?" Ndipo akacheka kifichifichi.

175 Naye huyo—huyo Mtu akiwa ameketi pale, huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" akiwa kwenye hema. Vipi kuhusu hilo? Mnaona, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu," kwamba Mungu angejidhihirisha Mwenyewe katika mwili, mwili wa kibinadamu, tena. Mnaona, Mungu juu yetu, Nguzo ya Moto; Mungu pamoja nasi, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu; sasa Mungu ndani yetu, Roho Mtakatifu, katika siku za mwisho, katika mwili wa mwanadamu.

176 Ibrahimu alipitia siku nzima akiona ishara na maajabu ya Mungu, lakini kamwe yeye . . . Wakati tu alipoiona ishara hiyo, mara baada ya hayo Moto ulishuka na kuiteketeza Sodoma; ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu aliiona kwa Mungu kabla ya Moto kushuka, ishara ya mwisho ambayo Israeli waliikataa ilikuwa ni ishara ile ile.

177 Sasa kanisa la Mataifa limeufikia wakati wao, sasa tunamtazamia Masihi. Na kama hivyo ndivyo alivyotenda kabla ya hapo, katika siku hiyo, hana budi kutenda vivyo hivyo leo. Kama akituacha tuingie bila hiyo, basi Yeye si yeye yule, na basi hatendi vile vile, na Yeye ana upendeleo. Mnaona ninachomaanisha? Yeye hana budi kufanya jambo lile lile tena, kwa hiyo hiyo inamfanya Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

178 Ustaarabu umesafiri pamoja na jua, sote tunajua hilo. Ustaarabu wa kale kuliko wote ni Uchina na sikuzote . . . Na ustaarabu unapokuja, dhambi inalundikana, inaendelea kulundikana, na sasa umefika kwenye Pwani ya Magharibi. Kuna kizuizi cha sauti, au, pazia la chuma linalotenganisha mashariki na magharibi. Hakuna watu zaidi huko nje baharini, unaenda moja kwa moja hadi ufike mashariki tena. Nayo dhambi imekuja sikuzote.

179 Wakati Mhindi alipoishi hapa, hakuwa na dhambi, alikuwa na vita vidogo vya kikabila. Lakini nanii . . . wakati mzungu alipokuja, alileta wiski, wanawake, mauaji, kadhalika. Nayo dhambi sikuzote imelundikana. Na dhambi inapolundikana, Biblia ilisema, “Adui anapokuja kama mafuriko, Mungu atainua kiwango dhidi yake.” Neno hili la Mungu lingeinua kiwango, Neno lingedhihirishwa zaidi, kudhihirishwa zaidi.

180 Roho Mtakatifu alishuka kwanza kwenye Pwani ya Magharibi, mtu fulani mweusi mwenye makengeza, huko chini California. Roho Mtakatifu alishuka California kwa kunena kwa lugha. Ndipo ukaja uamsho wa uponyaji wa Kiungu, na sisi hawa hapa kwenye wakati wa mwisho. Haleluya! Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele. Mnaamini hilo? Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo.

181 Baba wa Mbinguni, tunashukuru kujua kwamba tunaishi katika siku hii ya mwisho, kabla tu ya Kuja kwa Mwenye haki, Mwanao wa ajabu, mtukufu na mwenye upendo, Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo, Yule tunayempenda. Na tunajua Biblia inazungumza juu ya kuonekana kabla ya Kuja, na kuna tofauti kubwa katika neno *kuonekana*, na kisha *kuja*.

182 Sasa, Baba, tunatambua ya kwamba Kanisa limepitia hatua ya kuhesabiwa haki, likapitia hatua ya utakaso, likapitia hatua ya kumpokea Roho Mtakatifu. Sasa mawe yanachongwa yapate kuingizwa kwenye huduma ya Yesu Kristo, yapate kuumana

moja kwa moja kulichukua Kanisa. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili, Baba.

183 Tuna furaha sana kwamba Wewe . . . tunaweza kukutumainia. Neno Lako lisemavyo ni kweli, haliwezi kushindwa kamwe kwa sababu Wewe ni Neno, na Wewe ulisema, "Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitashindwa kamwe." Ninaomba, Baba, usiku wa leo, kufunguliwa kwa uamsho huu. Nimekuwa nikizungumza kwa muda mrefu, ni kikundi kizuri cha watu kuwazungumzia.

184 Sasa, Mungu, tunatazamia uamsho. Tunatazamia maskini siku hizi, fupi, chache, usiku, tulizo nazo hapa, Wewe upate kutuma Moto kutoka madhabahuni. Watu hawa, Baba, wengi wao ni waaminio, walimpokea Roho Mtakatifu, hakika Roho Mtakatifu angelijua Neno. Nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utalithibitisha tena, usiku wa leo. Na ijulikane ya kwamba Wewe ni Mungu na wakati unakaribia. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

185 Mungu awabariki. Ninataka usikivu wenu wote kwa takriban dakika kumi. Tuna wakati mwingi sasa, tuna siku nne usiku za kuwaombea wagonjwa, tutawaombea wote. Ninaamini ya kwamba Billy alisema alisambaza kadi za maombi. Mia moja? Mia moja? A? Alisambaza kadi mia moja za maombi, za A. Tutamwombea kila mmoja wao. Lakini sasa, hatuwezi kuwaleta wote hapa kwa wakati mmoja, wala hatuna wakati wa kuwaleta wote usiku wa leo. Huenda ikakubidi kusubiri kwa muda kidogo zamu yako ipate kuitwa.

186 Lakini vipi kama ilikubidi kwenda kwa Mayo Brothers na kungojea uone shida yako? Huenda ukangojea miezi mitatu au minne kabla ya kupewa miadi. Halafu ukiingia, unakaa mle ndani kwa wiki moja au mbili, watakufanyia uchunguzi kwelikweli, na kama wakiupata, wanakwambia, ndipo basi uko tu mahali ulipoanzia, ila tu unajua kinachokusumbua. Unaona? Lakini huwezi kumngojea Mungu siku chache tu, ama saa chache, dakika chache.

187 Tuwe askari ha—halisi kweli, kila mmoja wetu avae silaha zote za Mungu sasa, na kusimama papa hapa na kungojea kama askari halisi.

188 Sijui kwamba atalifanya hili, lakini angalieni hapa, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Kwa udhahiri kadiri nilivyojaribu kuufanya, mimi ni . . . Mimi si mtu mwenye elimu. Usemi wangu ni mbaya, nami nina sauti mbaya, wa—wala hakuna kitu kunihusu mimi ambacho ni chema. Lakini mimi . . . Mnaona? Lakini endapo Mungu ataninii tu . . . Yale niliyowaambia, mnayaamini kuwa ni kweli? Mnaona, hivyo ndivyo mngemjua Yesu? Vema.

189 Hebu tuite baadhi ya kadi hizi za maombi. Hebu tuanzie tu kutoka namba moja. Ni nani aliye . . . ? Ukiweza, simama

sasa, ninapoita namba yako. Namba moja. Nani aliye na kadi ya maombi . . . ? Hiyo ilikuwa herufi gani? [Mtu fulani anasema, "A."—Mh.] Ati A. H? ["A."] A. A, namba moja, inua mkono wako, yeyote aliye na hiyo kadi ya maombi. Huyu mama hapa? Utaendaje, utashukaje . . . ? Namba mbili. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba mbili? Kadi ya maombi A, namba mbili. Huko nyuma? Sawa. Njoo papa hapa, mama, moja kwa moja kuzunguka hivi.

190 Namba tatu. Vema, mama, njoo moja kwa moja hivi. Namba nne, namba nne, waweza kuinua mkono wako, yeyote aliye nayo? Ni huyo mama? Sawa. Nne. Inua mkono wako, basi sisi . . . Mimi na Ndugu Borders tunaangalia. Namba nne, namba tano. Hapa? Sita. Vema, sawa chukua tu mahali pako moja kwa moja karibu . . . Namba saba, namba saba. Sawa. Namba nane. Ninafanya hivi, kuwazuia kushindana. Nane, tisa. Nani ana tisa? Nambari tisa.

191 Ikiwa huwezi kusimama sasa, acha tu mtu . . . mwambie mtu aliye karibu nawe, inua mkono wako, tutakubeba hapa juu, tutahakikisha kwamba utafika hapa. Sema—sema, kama mtu angesema *tisa* kwa Kihispania, unasemaje? [Mtu fulani anasema, "Nueve."—Mh.] Nueve? ["Nueve."] Nueve, tisa, namba tisa. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane. Namba tisa. Samahani, samahani, Dada. Namba tisa.

192 Namba kumi, kumi na moja. Njoo moja kwa moja hapa chini, dada. Kadi ya maombi kumi na moja. Je, mama huyo aliyesimama hapo ni kumi na moja? Kumi na mbili, kumi na tatu. Njoo moja kwa moja . . . Kumi na tatu, kumi na nne, kumi na nne. Sikuiona, siamini. Kumi na nne, kumi na tano. Kadi ya maombi kumi na tano, unaweza kuinua mkono wako? Kadi ya maombi . . . Hiyo ni kumi na tano? Tuna wangapi? Tuanzie papo hapo.

193 Sasa, kila mmoja wa watu hao angeweza kuamka na kutembea. Sasa, kwa mfano, sioni vilema wowote walioketi hapa, isipokuwa iwe ni yule mama aliyeketi pale kwenye—kwenye kiti. Kama ningesema huyo mama, ambaye, ninamjua, kama ningesema huyo mama ni mlemavu, vema, mngesema, "Hakika." Vipi kuhusu huyu mama aliyeketi *hapa*? Huyu *hapa*? Sasa, ni wangapi wenu ambao hawana kadi ya maombi mkutanoni, na hata hivyo mnaamini Yesu Kristo atawaponya? Hebu tuone mkiinua mikono yenu. Nyinyi nyote. Kila mtu aliye na kadi ya maombi. Kila mahali tu.

194 Sasa, angalieni, wakati wakiwakusanya watu hao pamoja, ningetaka kupata usikivu wenu. Siku moja kulikuwa na mama mmoja aliyepitia kwenye ku—kundi la watu. Na tuseme, hakuwa na kadi ya maombi, lakini aliamini kama angeweza kugusa upindo wa vazi Lake, atakuwa mzima. Ni wangapi wanaojua hiyo hadithi? Sote tunaijua, hakika, hiyo ni sawa. Kama

angeweza kugusa upindo wa vazi Lake . . . Sasa, naye akapenya, na akaligusa vazi Lake.

195 Na sasa, siamini Yeye angeweza kuuhisi kimwili, kwa sababu vazi la Wapalestina hushikilia . . . li—lina vazi la ndani, halafu ni joho, linapwaya namna *hiyo*, naye aligusa upindo wake.

Ndipo Yesu akageuka, akasema, "Ni nani aliyenigusa Mimi?"

196 Naye Petro akamkemea, halikusikika kama swa—swa—swa . . . si swali la busara, kasema, "Mbona, Bwana, kila mtu anakugusa." "Aloo, Rabi, nimefurahi kukuona." "Aloo, hapo, Nabii, tuna furaha kukuona." "Aloo," namna hiyo.

Naye akasema, "Ni nani aliyenigusa Mimi?"

Vema, kasema, "Unaongea kiajabu." Akamkemea Yesu.

197 Yesu akasema, "Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu. Uweza" nguvu "zimenitoka. Nimekuwa dhaifu." Naye akatazama kote katika hilo kusanyiko, ndipo akamwona maskini mwanamke huyo. Ni wangapi wanaojua shida yake ilikuwa nini? Alikuwa anatokwa na damu, na amekuwa nayo kwa miaka mingi. Naye akasema, "Imani yako imekuokoa."

Sasa, neno la Kiyunani hapo, *Sozo*, ambalo linamaanisha vile vile kwa kimwili na kwa . . . "Imani yako imekuokoa."

198 Sasa, Biblia ilisema ya kwamba "Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu, sasa hivi," Mnaamini? "Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Hiyo ni kweli?

199 Vema, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, angetendaje? Sawasawa na alivyofanya wakati huo. Hilo lingemfanya Kuhani Mkuu yeye yule, jana, leo, na hata milele, mnaona. Ninii tu, hakuna njia ya kujiepusha nalo. Ninii . . . Kama Biblia inatangaza jambo lolote, ni ukweli. Je, hiyo ni kweli?

200 Sasa, ni nini—ni nini kinachotokea hapa? Sasa, karama . . . Sasa, Biblia ilisema, kwa ajili ya ndugu hawa wahudumu, Biblia ilisema kwamba Mungu ameweka kanisani karama tano tofauti. Hiyo ni kweli? Mungu ameweka. Sasa, kuna karama tisa katika—katika kanisa la mtaa moja tu au lingine, lakini karama tano za huduma, mitume, manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti. Je, hiyo ni kweli? Karama tano za kiroho. Sasa, karama hizo ni kwa ajili ya kukamilishwa kwa kanisa, kuweka kanisa katika utaratibu, wachungaji, na walimu, na wainjilisti, na manabii, na kadhalika. Sasa, ni karama.

201 Sasa, haidhuru watu hawa hapa wamejaliwa kuhubiri kiasi gani, hamna budi pia kuamini wanachohubiri, au haitafaa kitu hata kidogo. Wangeweza tu kuhubiri na kuendelea, na kuendelea, hutaokolewa kamwe, ungekufa papo hapo kwenye kiti, na upotee, hiyo ni kweli, huku umeketi papo hapo. Hiyo ni kweli, huna budi kuamini wanachosema. Vema, haijalishi Mungu angefanya nini hapa kwa njia ya karama ya unabii, huna budi kuiamini pia.

202 Alipokuwa ndani ya Kristo . . . Naye yuko katika Kanisa Lake sasa. Sasa, alipokuwa ndani ya Kristo, alikuwa tu mahali pamoja. Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, "Kazi . . . Yeye . . ." Yohana Mtakatifu 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Je, hiyo ni kweli? "Kazi . . . Aaminiye," kwa sababu gani? Neno liko ndani Yake. Mnaona? "Yeye aniaminiye Mimi, kazi ambazo Mimi . . . Zaidi ya hizi . . ." Najua la King James linasema "kubwa zaidi," lakini huwezi kuwa mkuu zaidi, tafsiri yake sahihi katika asili ni "nyingi zaidi," kwa sababu Yeye aliwafufua wafu, aliyakomesha maumbile, alifanya kila kitu kikamilifu.

203 Kwa hivyo ni nyingi zaidi tu, kwa sababu yule—yule Roho aliyekuwa ndani Yake, siku ya Pentekoste, ile Nguzo ya Moto iliyofanyika mwili, ikakaa kwetu, ilikuwa imerudi tena na kujigawa Yenyewe, kwenye siku ya Pentekoste, miongoni mwa wanafunzi, "Ndimi za Moto zikakaa juu ya kila mmoja wao." Mungu akijigawa Mwenyewe miongoni mwa watu Wake, ili kwa pamoja tuweze kuwa kitengo cha Mungu. Tunapaswa kusimama kama . . .

204 Sasa . . . Sasa, kama . . . Ninaamini kila mtu katika mstari huo wa maombi ni mgeni kwangu. Sininii . . . Hakuna mtu hapa ninayemjua, nje ya Ndugu Borders. Na—na sasa, simaanishi . . . Huenda nimekutana nanyi ndugu kwenye mikutano, lakini kujua tu ninyi ni nani . . . Na ninaamini huyu ni—huyu ni yule ndugu kutoka Ohio hapa, anayeketi moja kwa moja . . . wala siwezi kulikumbuka jina lake sasa, Fritzinger, kutoka Ohio, Ndugu na Dada Fritzinger wanaoketi hapo, kutoka Ohio. Huyu ni Ndugu na Dada Dauch wanaoketi hapa kutoka Ohio. Nami ninamjua Ndugu Sothmann, naye Ndugu Wood yuko hapa ndani mahali fulani, wale wauza vitabu, hao, siwaoni, sijui walipo.

205 Lakini sasa, kama Roho Mtakatifu atakuja na kuthibitisha yale niliyosema usiku wa leo kuwa ni kweli, basi kungekuwa na mambo mawili. Ingewaonyesha ya kwamba Yesu Kristo angali hai (Hiyo ni kweli?), yeye yule jana, leo, na hata milele. Maana kama mwanadamu, siwezi kufanya kazi hizo, inamhitaji Yeye kuzifanya. Kwa hiyo mngejua itabidi iwe ni Yeye.

206 Na jambo lingine ingeonyesha, ni kwamba wakati umekaribia, hiyo ni kweli, wakati, ishara ya mwisho ambayo Israeli walipokea, ishara ya mwisho ambayo—ambayo walipokea, Lutu, Ibrahimu, kabla ya yale maangamizi. Kila kitu kinaonyesha sasa hivi tuko katika vivuli vya Kuja Kwake.

207 Kwa hiyo rafiki mwenye dhambi, kama uko hapa usiku wa leo, naye Mungu anathibitisha ya kwamba Yeye yuko hapa miongoni mwetu, si uje na kumkubali kama Mwokozi wako? Wewe fanya hivyo.

208 Sasa, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho hapa ndani chini ya udhibiti

wa Roho Mtakatifu. Sasa, msisogeesogee, tulieni, iweni na kicho, ombeni. Na ninyi huko nje sasa, ombeni tu, na kusema sasa, "Nitaninii . . . Bwana, mhudumu huyo hanijui, lakini nijalie niguse vazi Lako, nijalie nikuguse Wewe, kisha useme kupitia kwake, nitajua ni Wewe, unaona, maana huyo ni Wewe ukitenda kupitia Kanisa Lako kama alivyosema ulikuwa." Vema. Hebu tuchukue . . .

209 Haya ni matembezi makubwa hapa. Sasa . . . (Asante.) Huyu hapa mwanamke ambaye hatufahamiani kabisa. Sasa, ninawatakeni myaweke Maandiko haya usiku wa leo akilini mwenu, mtakapoenda nyumbani, someni Yohana Mtakatifu 4, hili hapa, mwanamume na mwanamke wanakutana kwa mara ya kwanza. Mnaona, papa hapa, kama vile tu katika wakati wa Biblia, Bwana wetu Yesu alikutana na mwanamke asiyemjua, mwanamke huyo hakumjua.

210 Sasa, mwanamke huyu, si—simjui, sijawahi kumwona. Kwa hiyo yeye ni mwanamke fulani tu anayesimama hapa. Sasa, anaweza kuwa . . . Labda yeye ni—ni kafiri mbaya kabisa, huenda akawa ni Mkristo, huenda akawa ni m—mdanganyifu, huenda akawa ni . . . huenda akawa ni mgonjwa, huenda ikawa amesimama kwa niaba ya mtu mwingine. Huenda ikawa ni matatizo ya nyumbani, huenda ikawa ni matatizo ya kifedha. Sijui mimi, lakini Yeye anajua.

211 Sasa, kama nikija, na kusema hivi, "Utukufu kwa Mungu . . . " Hiyo ni . . . Sasa mimi si . . . Kumbukeni, huyo ni Roho Mtakatifu, ndugu, anayesema hivyo. Kama ningesema, "Utukufu kwa Mungu, Dada, Bwana alinituma kuwaombea wagonjwa. Unaniamini?"

Angesema, "Ndiyo, ninakuamini."

"U mgonjwa?"

"Ndiyo."

"Una shida?"

"Ndiyo."

"Ni kitu gani?"

Angesema, "Naam, na—nafa kwa kansa," au "Nina TB," au—au kitu kama hicho.

212 Ningesema . . . niweke mikono yangu juu yake, niseme, "Yesu alisema, 'Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.' Alisema, 'Weka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.' Haleluya! Nenda ukaamini." Hiyo inaweza kuwa ndivyo. Angeenda na kuponywa pia, kama akiamini.

213 Lakini sasa, hebu tubadilishe hilo sasa, tumekuja mbele zaidi kidogo. Sasa, vipi kama Yeye akisimama hapa na kumwambia jambo ambalo . . . acha amwambie shida yake. Amwambie jambo ambalo amefanya, ama jambo ambalo

hakupaswa kufanya, ama kama . . . kile alicho. Basi ikiwa—ikiwa yaliyopita ni ya kweli, atajua kama hiyo ni kweli au la, na halafu, kama Yeye anaweza kumwambia yale ambayo yamekuwako, na kisha atamwambia yale yatakayokuwako, hilo limelipata basi, sivyo? Ndivyo—ndivyo hivyo. Mnaona? Hilo linalitoa nje lote. Mnaona? Ndivyo hivyo. Je, mngeamini? Kila mtu anaamini? Vipi kuhusu huko juu kwenye roshani, mngeamini, enyi marafiki, huko nyuma kabisa?

214 Sasa, kumbukeni, hatuko hapa kama onyesho la jukwaani, hili si jambo la kuigiza, huku ni kujaribu kumwakilisha Mungu wa Biblia. Nao Ukristo unavutia, kama ukihubiriwa kwa urahisi na ukweli wake, mnaona, si kufanya maneno mazito, makubwa, ya kiburi, ya kielimu. Kama Paulo alivyosema, "Sikuja kwenu namna hiyo, bali katika nguvu na ufufuo wa Kristo, ili imani yenu iwekwe msingi katika hayo, ya kwamba Yesu Kristo yu hai." Na basi kama Yesu Kristo yu hai, na anaweza kunena na dada yetu hapa, ama, mwanamke huyu, na kunena kuhusu hilo, basi Yeye ni yeye yule tu huko nje kwako kama alivyo hapa jukwaani, ama popote pale. Unaona? Unaamini hilo sasa?

215 Sasa, kuzungumza naye tu kwa muda kidogo, ili tu kuwasiliana na roho yake. Sasa, huyu hapa mwanamume na mwanamke tena, wanakutana kwa mara ya kwanza maishani, kama . . . Sasa, bila shaka, kuna watu wengi huko nje wanaoomba, na kama mimi . . . Baada ya kupata upako hapa, ndipo Hiyo inaondoka na kwenda kote jengoni. Bila shaka baada ya kidogo kupata siku chache usiku, na kila mtu anafikia, mnajua, kuizoea, mambo kama hayo . . .

216 Sasa, sisi tukiwa ni wageni wala hatufahamiani, kama . . . Lakini Kristo yuko hapa, Yeye ndiye Ufufuo, Yeye—Yeye—Yeye alisema, "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima." Basi anaishi milele, anaweza kutuombea daima.

217 Na huku nikihisi Roho yake ya Kikristo ikinikabili sasa, ikinijia, inanifanya kujua ya kwamba huyo—huyo hapo Mkristo. Mnaona? Roho yake imekaribishwa, yeye ni Mkristo. Na kwa hiyo basi, mnaona, kwamba pale, sasa huyu hapa ndugu na dada wa Mungu yeye yule. Mnaona? Nanyi ni wahitaji, naweza kuona wewe ni—wewe ni mhitaji, na una haja ya kitu fulani.

218 Na sasa, Baba wa Mbinguni tayari ameweka pesa kwenye benki kwa ajili yako alipomtoa Mwanawe. Lakini sasa, jambo ni kwamba, kukufanya kuwa na imani ni kujua ya kwamba Yeye yuko hapa, amesimama hapa, kwa sababu unajua halina budi kupitia kwenye nguvu fulani. Hiyo ni kweli.

219 Sasa, kama watu bado wanaweza kunisikia, moja kwa moja juu ya huyu mwanamke, kama mnaweza kuona, kuna Nuru ya zumaridi-kijani. Huyu mwanamke anatambua vizuri sana jambo fulani linaendelea, kwa sababu ni hisia tamu, tamu sana, takatifu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Anatiwa mafuta

sasa na Roho wa Mungu. Naye mama huyo anasumbuliwa sana na fadhaa, fadhaa mbaya sana, na . . .

220 Hizo huja sikuzote. Ni kwa nini hivyo? Sikubahatisha hilo. Mnaona? Unafikiri nilibahatisha hilo, sikubahatisha. Unaona? Huko hakukuwa kubahatisha, hakuwezi kuwa kubahatisha. Lakini ni ukweli, lolote lile lililokuwa. Sijui lilikuwa nini, hiyo kanda inalo. Lakini lolote ililosema lilikuwa kweli.

221 Hebu kidogo tu. Anaonekana kuwa mtu mzuri, ongea tu . . . Naam, hili hapa, fadhaa, fadhaa nyingi kweli, nayo hiyo fadhaa ni mbaya sana hata inakuuma, unaumwa. Halafu una tatizo lingine, henia ya kiwambo hapa ndani. Hiyo ni kweli. Hiyo si ni kweli? Na si ajabu, unapaswa kuamini, ukiwa mhudumu, mwanamke mhubiri. Hutoki kwenye nchi hii, unatoka Missouri. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Unaamini sasa? Nenda, na yote yatatoweka. Nenda na uamini kwa moyo wako wote. Mungu akubariki, dada yangu. [Dada huyo anasema, "Ndugu Branham, Mungu aliniambia nitakuona nitakapokuja."—Mh.] Asante.

222 Sasa, mnaamini? Ni wangapi wanaoamini? Mbona, hakika. Kamwe huwezi kujizuia kuamini, sivyo? Aminini tu, hilo ndilo tu mnalopaswa kufanya. Aminini tu.

223 Sasa, hatufahamiani. Unaamini Roho Mtakatifu yuko hapa? Sasa, ninachopaswa kufanya, Dada, sina budi kukuhurumia, wajua. Inabidi iwe ni kitu ambacho nakuhurumia, kuna mengi sana ya Ukristo huu wa macho baridi siku hizi, mkavu na umekatwa. Huna budi kuwahurumia watu. Sasa, hebu kidogo.

224 Kulikuwa na mwanamke. Alisema alikuwa ameomba, na ya kwamba Mungu alimwambia ya kwamba angekuja, ama, ataniona hapa. Endelea tu kuamini. Hilo ni zuri sana, kama mnaweza kuendeleza hilo, wimbi hilo halisi la imani linalotoka kwenye kusanyiko basi, hilo ni zuri. Endeleeni tu kuwazia sasa, endeleeni tu kuamini. Msitie shaka. Liwekeni moyoni mwenu sasa.

225 Mwanamke huyu, hapa, anaomba, na anataka kuombewa, kutokana na uvimbe kichwani mwako, hiyo ni kweli, chini ya nywele zako ambapo umejificha. Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini? Vema. Basi nenda na huo uvimbe utakuacha . . .?. . . Amini tu. Amini kwa moyo wako wote. Aminini sasa, msitie shaka. Tulieni tu kabisa na mwe na kicho sana.

226 U hali gani? Hatufahamiani pia, naamini. Bwana Yesu anatujua sote wawili, anajua kilichokuleta hapa, anajua yote kukuhusu, mimi sijui, lakini Yeye anajua. Lakini ikiwa Bwana Yesu atanifunulia shida zako, utaamini haina budi kutoka Kwake? Hiyo ni kweli? Vema. Amini tu kwa moyo wako wote.

227 Sasa, kweli si wewe mwenyewe, unamjali mtu mwingine. Hiyo ni kweli. Ni mwanamume, na mwanamume huyo ni mkwe wako, naye mkwe wako ana vidonda, nawe unataka nimwombee.

Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Chukua leso hiyo ukaiweke juu yake. Sasa, nenda ukiamini sasa.

Unaamini kwa moyo wako wote? Usiwe na shaka kamwe, amini. Sasa, kuwa na kicho sana sasa. Amini, usiwe na shaka hata kidogo, amini.

228 U hali gani? Hatufahamiani, nadhani? Lakini Bwana Yesu anatujua sote wawili. Sasa, kupindapinda, kunatokana tu na hayo maono. Mnaona? Ni . . . Kama maskini mwanamke mmoja alifanya nguvu zimtoke Bwana na Mwokozi wetu, ingefanyaje kwangu mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yake? Unaamini kama Bwana Yesu atanifunulia jambo fulani kukuhusu, utaliamini. Sasa, kuwa tu na kicho sana sasa. Kamwe usiwe na shaka.

229 Una matatizo kadhaa, jambo moja ni kibofu kilichoshuka. Hiyo ni kweli, sivyo? Na jambo lingine, una ki—kivimbe, nacho kiko tumboni. Hiyo ni kweli, sivyo? Vema. Unaamini sasa kwamba utakuwa sawa? Basi pitia hapa na useme, "Asante, Bwana Yesu." Usiwe na shaka kabisa moyoni mwako, unaweza kupata ulichoomba. Amini tu sasa unapokuja.

230 U hali gani, Dada? Unaamini kwa moyo wako wote? Vema sasa, tumezaliwa labda maili kadhaa mbalimbali, na miaka mbalimbali, na sisi hawa hapa tunakutana kwa mara yetu ya kwanza.

231 Kwa namna fulani siwezi kumshika huyo kwenye kusanyiko. Kuna mtu huko nje anaomba. Sasa, ni mwanamume, lakini siwezi kujua alipo, inaendelea kuja. Ni mtu huyu anayeketi papa hapa akinitazama moja kwa moja kwenye kidole changu hapa, anaugua yabisi kavu, ameketi huko nje. Naam, bwana, wewe. Una yabisi kavu. Amini kwa moyo wako wote. Inua mkono wako juu. Vema, amini sasa kwa moyo wako wote, hiyo yabisi kavu itakuacha.

232 Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Aligusa nini? Niambieni alimgusa Nani. Yeye yuko futi arobaini kutoka kwangu au zaidi. Alimgusa huyo Kuhani Mkuu. Mwulizeni kama hakuwa ameketi pale akiomba. Hiyo ni kweli, bwana? Amini tu kwa moyo wako wote. Hilo tu ndilo unalopaswa kufanya sasa, amini.

233 Hatufahamiani, nilisema. Nisingeweza kujizuia, mtu huyo aliendelea kuja mbele yangu hapa, nami nikamwona, alikuwa mlemavu mnaona na hivyo, kumbe ilikuwa ni yabisi kavu. Atakuwa sawa kama ataendelea kuamini tu.

234 Sasa, kama Roho Mtakatifu . . . Unajua itabidi iwe ni nguvu fulani ku—kupeleka hii. Na sasa, Biblia ilisema, "Neno la Mungu ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo." Na hiyo ndiyo sababu Yesu aliweza kutambua walichokuwa wakifanya, na kadhalika, kwa maana Yeye alikuwa Neno. Kisha akasema, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu . . . " Mnapata

hilo wazo sasa? Hiyo ni kweli. Hasa. Iwapo utaamini hilo kwa moyo wako wote, hiyo ngiri itakuacha. Unaamini?

235 Nataka kukwambia jambo lingine. Wewe ni mtu mzuri, na una haja ya kina moyoni mwako unayotaka kuniomba niiombee, nawe ulihofu nitakupita. Siyasomi mawazo yako, lakini ulitaka kuniambia kitu, sivyo? Unataka nikwambie, kabla hujaniambia? Ni kwa ajili ya mumeo. Naam, bwana. Naye anasumbuliwa na ugonjwa wa uvimbe. Hiyo ni kweli? Amini kwa moyo wako wote, na uende ukashuhudie, na uweke mikono yako juu yake, na kadhalika, nao utamwacha na atakuwa mzima. Amina.

236 Unaamini? Amina. Amini. Unataka kula chakula chako cha jioni kwa amani? Maskini tumbo lenye fadhaa likuache? Ondoka moja kwa moja jukwaani, kula chakula chako cha jioni, useme, "Asante, Bwana Yesu."

237 U hali gani? Unaamini? Unaamini anaweza kuponya ugonjwa wa moyo? Unaamini anaweza kuponya ugonjwa wako wa moyo? Vema. Basi endelea moja kwa moja, useme, "Asante, Bwana Yesu, kwa—kwa ajili ya kuuponya ugonjwa wangu wa moyo, nami ninaenda, kuisahihisha."

238 Sasa, niliposema hivyo kuhusu mama huyo, hisi ya kigeni sana ilikujia, maana ulikuwa na ugonjwa wa moyo pia. Unakumbuka nilisema *ulikuwa* nao. Endelea tu. Unaona? Kuwa tu na imani.

239 Jambo la ajabu, amini kwa ajili ya mtoto huyo nao utamwacha pia. Vema. Je, unaamini hilo? Vema. Yeye yuko karibu. . . Nataka kuweka mikono yangu juu ya huyo mtoto.

Shetani, mfungulie huyo mtoto.

Katika Jina la Yesu Kristo, na aponywe. Usiwe na wasiwasi juu yake. Nenda, ukiamini, utaondoka, aponywe.

240 Mama huyu ametiwa uvuli na kansa, lakini kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya. Unaamini? Vema, bwana, pita moja kwa moja, ukisema, "Asante, Mungu mpendwa." Ninaweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya, katika Jina la Yesu Kristo.

241 Nitachunguza tu mmoja mara moja, unaona. Vipi kama sikukwambia lolote, nikuwekee mikono tu? Unaamini ungekuacha? Ungeamini? Sawa, njoo. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina. Sawa, acha niangalie. . .?. . . Amini.

242 Je, ungeamini jambo lile lile? Nikikuwekea tu mikono, basi utaamini? Vema. Mungu akubariki. Katika Jina la Yesu Kristo, na aponywe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.

243 Vipi kama ningekwambia jambo lile lile, litakusaidia? Sasa, una shida ya wanawake, lakini jambo lako kuu ni ugonjwa wa moyo ambao una wasiwasi nao namna hiyo, kwa sababu ni wasiwasi moyoni mwako.

244 Hebu kidogo, dakika moja tu. Jambo fulani lilitokea. Kila mtu awe na u- . . . uchaji kwelikweli sasa. Iko kwenye kusanyiko. Hii hapa. Ni yule mama anayeketi pale, akimwombea mume wake ambaye ana ugonjwa wa moyo. Ukiamini kwa moyo wako wote, mumeo atapona. Usitie shaka, amini kwa moyo wako wote.

Wako umekwisha. Amini tu sasa wala usiwe na shaka.

245 U hali gani? Unaamini Mungu anaweza kuniambia una shida gani? Nifanye nisifanye, Yeye afanye asifanye, hasa, ungeamini kwa vyovyote vile, sivyo? Ungeamini. Kama nikikuwekea tu mikono, unaamini kwamba hicho kisuka- . . . Hivyo . . . Ni kisukari. Nilikwambia, sikumaanisha . . . Nilikuwa nikiangalia kupimwa huko kwa damu, ndivyo ilivyokuwa, kupimwa kwa sukari pale nikaona kwamba ni . . . Unaamini kwa moyo wako wote?

246 Mtu huyu anayeketi moja kwa moja nyuma, naam, papo hapo nyuma ya Ndugu Sothmann hapo, ana shida ya miguu yake. Kama utaamini kwa moyo wako wote, bwana . . . Una imani nyingi kuliko ulivyowazia ulikuwa nayo. Inua mkono wako. Vema. Imekwisha ikiwa utaamini. Amina. Hebu tuseme, "Bwana asifiwe."

247 Hiyo si ilikuwa ni ajabu, kwamba alirudi moja kwa moja wakati ule ule? Mnaona? Kwa nini Hiyo ikamwambia wakati ule ule pamoja na wewe? Nilitaka tu ujue kwamba ulikuwa na imani pia. Amina.

Mnampenda? Aminini sasa, msiwe na shaka.

Mama aliyeketi pale *pale* ana shida ya miguu yake pia. Ukiamini kwa moyo wako wote, unaweza kupokea uponyaji wako.

248 Na yule aliyeondoka . . . akaketi moja kwa moja *pale* nyuma ana ugonjwa wa moyo. Naam, bwana. Unaamini kwa moyo wako wote? Wewe . . . Naam. Una kadi ya maombi? Una kadi ya maombi? Haitakubidi kuitumia sasa, imani yako imefanya hivyo.

Unaamini?

249 U hali gani, Bwana? Hatufahamiani, lakini unaamini kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida zako? Je, wewe . . . Je, . . . Hiyo ingekuwa . . . Nisingeweza kukuponya, bila shaka, unajua hilo, mimi ni—mimi ni ndugu yako. Nisingeweza kukuponya, lakini Yeye tayari amefanya hivyo, anataka tu ujue kwamba Yeye yupo. Unaamini hilo? Vema, bwana. Bwana awe pamoja nawe.

250 Una ugonjwa wa figo, ugonjwa wa kibofu, ndio kwanza ufanyiwe upasuaji. Hiyo ni kweli. Hiyo si ni kweli? Hutalazimika kuwa nayo tena. Nenda, ukiamini, ukapone, katika Jina la Bwana Yesu. Mungu akubariki. [Ndugu huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Amina.

Anataka kumsifu Bwana. Alisema nilimwita wakati mmoja mahali fulani, naye akaponywa na angali anao uponyaji huo leo hii, anaendelea vizuri.

251 Ni wangapi wanaoamini? "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Mnaamini? Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Je, Neno Lake lingali ni lile lile? Sasa, ni waaminio wangapi walio hapa ndani? Inua mkono wako.

252 Sasa, hivi Yesu hakulipa Kanisa Lake agizo hili la mwisho, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio"? Waaminio, sivyo? Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, itakuwaje? Watapona.

253 Sasa, ninawatakeni mwekeane mikono, juu kwenye roshani, chini hapa ndani. Kila mmoja wenu ninyi waaminio, wekeaneni tu mikono. Hiyo ni kweli. Mtu fulani tu anayeketi karibu nawe hapo, mbele yako, nyuma yako, ama mahali fulani, wekeaneni tu mikono, ninyi ni waaminio. Ili kwamba, nataka muone sasa ya kwamba si hapa juu tu, Yeye yuko huko nje, Yuko kila mahali. Unaamini? (Leso . . .?. . .)

254 Huko juu kwenye roshani, mko tayari, kuwekeana mkono? Sasa, inamisheni vichwa vyenu kila mahali. Wekeaneni tu mikono na mwinamishe vichwa vyenu. Sasa, Yesu wetu anayewathibitishia ya kwamba yuko hapa sasa hivi, Yuko hapa, Roho Wake. Ulisema, "Tunataka kumwona Yesu." Huyu hapa, akitenda kazi moja kwa moja kupitia Kanisa Lake, watu Wake.

255 Sasa, nisingeweza kufanya hivyo mimi mwenyewe, hiyo ni imani yenu pia. Haidhuru nina imani kiasi gani, huna budi kuwa na imani pia. Mnaona? Nayo imani yako ilimgusa, na kwa karama aliyonipa, ananena tu Maneno Yake kwenu. Mnaona?

256 Sasa, ninanukuu Maneno Yake kutoka katika Biblia, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya." Sasa, nataka kila mmoja wenu . . . Usijiombee mwenyewe, maana mtu ambaye amekuwekea mikono yao anakuombea. Wewe waombee.

257 Sasa, ninakutaka uombe jinsi ufanyavyo kanisani mwako. Anza tu kuomba sasa, kwa ajili ya mtu huyo, ukisema, "Bwana Mungu, mimi ni mwaminio, najua kuwa Wewe upo. Ninaweka mikono yangu juu ya jirani yangu hapa, nami ninataka waponywe." Nao wanakuombea, nami nitaombea kila mmoja wenu.

258 Baba yetu wa Mbinguni, tunakaribia sasa, tena, baada ya ibada, kuona ya kwamba unafanya mambo yote vema. Tunaamini juma hili ya kwamba viwete, walemavu, vipofu, waliopooza, vilema wataponywa kwa nguvu Zako, na watapata afya. Mioyo ya wenye dhambi itaoshwa kwa Damu ya Yesu Kristo. Kutokuamini kutafifia kwenye uamsho mkuu wa nguvu za Mungu, Mwana wa Mungu.

259 Na sasa, waaminio hawa, hapa, wamewekeana mikono. Naye Yesu, ambaye yuko kila mahali, na umethibitisha ya kwamba Wewe uko hapa katika ukumbi huu, usiku wa leo, Wewe uko hapa. Tumewekeana mikono, nami ninawaombea, wanaombeana. Na sasa, Baba, tunakuja kuamini ya kwamba Wewe utafanya kila ugonjwa kutoweka mahali hapa, kila mgonjwa aponywe.

260 Shetani, tunakugeukia wewe, ewe mwanafalsafa mkuu, mwerevu, msomi, mdanganyifu, unayejaribu kulipinga Neno la Mungu, Neno limedhihirishwa. Tunakuja kukabiliana na changamoto yako katika Jina la Yesu Kristo, Yeye aliyesulubiwa, akafa, akafufuka tena siku ya tatu, akashinda kila ibilisi, kila pepo, kila nguvu ulizopata kuwa nazo, akakunyang'anya kila haki ya kisheria uliyokuwa nayo, maana Yeye alilipa gharama, na kulinunua tena Kanisa Lake kwa ukombozi. Na, usiku wa leo, sisi ni watu waliokombolewa, nawe umeshindwa vita.

261 Toka ndani ya watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo, waache. Mikono mitakatifu ya waaminio imewekwa juu ya waaminio wengine, nawe umeshindwa vita, naye Kristo yuko hapa kuthibitisha amefufuka katika wafu baada ya miaka elfu mbili na angali hai hata milele. Tunakuapisha, kwa Mungu aliye hai, waache watu hawa, toka ndani yao katika Jina la Kristo.

262 Kila mwanamume na kila mwanamke, kila mwaminio sasa, huku mmewekeana mikono, mmejifungia ndani, aminini. Kristo yu karibu sasa, mmemwona akitenda kazi jukwaani, huko nje kwenye kusanyiko kwa Neno Lake lisiloweza kukosea. Maombi ya imani yameombwa kwa njia ile ile aliyonenea, akichukua midomo ya mwanadamu na kutenda kazi, Mwenyezi Mungu akifunua, akijionyesha Mwenyewe ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

263 Ninyi hamko miongoni mwa kundi la wasioamini, ninyi si kundi la watu wenye akili, mmeketi kati ya watakatifu, watauwa, mmefufuka pamoja na Kristo, mmeketi katika mahali pa Mbinguni. Wanaume na wanawake watakatifu wamewawekea mikono, wakiomba maombi ya imani, Shetani ameshindwa katika Jina la Yesu Kristo, Damu imetetewa.

264 Sasa, vunjilieni mbali juu yenu, kwa imani, giza hilo ambalo lingewafanya mtilie shaka jambo moja la Uwepo wa Mungu, ndipo uponyaji wenu utakuwa wa hakika. Fanyeni hivyo sasa, tunapoendelea kuinamisha vichwa vyetu, tukiwa tumefungiwa ndani pamoja na Yeye.

265 Basi tunataka kuimba, ikiwa mpiga kinanda atatupa tuni ndogo hapo, sauti ndogo, "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza." Endeleeni kuinamisha vichwa vyenu sasa, macho yenu yamefumbwa. Mwabuduni sasa. Weka mikono yako juu ya—ya jirani yako, weka mikono yako juu ya jirani yako sasa, huku umefungiwa ndani pamoja na Kristo.

266 Kila hitaji limetimizwa, kama tu vile ulivyoenda na kuziungama dhambi zako na ulikuwa umesimama juu ya maji, na mhudumu fulani mcha Mungu alikuwa amekushika mkono, alitaka kukubatiza, jambo lile lile. Neno likifanywa halisi, kudhihirishwa.

267 Mlisema, "Sisi tungetaka kumwona Yesu." Amejithibitisha Mwenyewe kati yenu, nilimwona, mlimwona; nilimhisi, Wewe ulimhisi. Huyu hapa, Yuko hapa.

Nampenda, nampenda

Kila mtu sasa, akiimba.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu (Kumbuka, wakati uliopita.)
. . . Kalvari (Wokovu kwa nafsi au mwili wako, wapi?) Mtini Kalvari.

Tena sasa, moyo wako wote.

Nampenda, nampenda . . . (Uhisi Uwepo Wake, nguvu Zake za uponyaji zikija ndani yako kwa sababu unamwamini?)
. . . alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Sasa, tunapouvumisha.

Nampenda, nampenda (Huo ni Uwepo Wake pamoja nawe.)
Kwani alipenda kwanza . . . (Sasa, amefanya nini hapa? Alinunua uponyaji wako. Alifanya nini?)
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

268 Sasa, wakati kinanda kikiendelea kucheza, wewe uliyehisi imani hiyo moyoni mwako . . . Haijalishi unajisikiaje, si jinsi unavyojisikia, wajua, kimwili, ni imani yako. Ulijisikia moyoni mwako ya kwamba Mungu amekuwa pamoja nawe mpaka umeona, unaliona Neno Lake ambalo limehubiriwa, likidhihirishwa, unajua hilo bila shaka yoyote ya kwamba Kristo mkuu wa kimbinguni aliyefufuka katika wafu, miaka elfu mbili iliyopita . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . angali hai, usiku wa leo, na mumu humu Kanisani Mwake. Nasi tunakaribia wakati wa mwisho.

269 Kama wewe si Mkristo, na ungependa kuwa Mkristo, naomba usimame tu kwa miguu yako na kusema, "Ninataka kumkubali kama Mwokozi wangu." Hivi mtasimama, wale ambao wangetaka kufanya hivyo wakati huu? "Nampenda. Kama anaweza kuja hapa, na kujua siri ya moyo, na kulifanya

Neno Lake halisi sana hata hakuna awezaye kulitilia shaka . . . " Liko papa hapa mbele yetu.

270 Ninawaangalia watu wawili wanaopaswa kusimama. Sasa, ninii tu . . . Mungu awabariki. Vema. Mungu akubariki. Simama tu, ewe jamaa mdogo. Vema. Mtu mwingine sasa, simama tu, useme, "Ninasimama mwenyewe kutoa ushuhuda, nataka kumkubali kama Mwokozi wangu. Ninamtaka, wakati nikiwa karibu Naye hivi, Uwepo Wake upo hapa, ninamtaka awe Mwokozi wangu."

271 Mtu mwingine? Njoo sasa. Mungu akubariki, kijana. Hilo ni jema. Simama kwa miguu yako na useme, "Nataka—nataka kulikubali. Nataka kuonyesha kwamba—kwamba ni . . . kwamba ninataka kuthibitisha kuwa niko tayari kumtetea." Mtu fulani kwenye roshani? Kidogo kuna giza huko juu. Amini kwa moyo wako wote.

272 Endapo wewe si Mkristo, je, utamkubali katika Uwepo huu? Hima sasa, unajua ya kwamba unajisikia kwamba unapaswa kufanya hivyo, simama. Vema. Sasa, wote wanaotaka kumkubali kama . . . Mungu akubariki. Mungu akubariki, Dada. Ajabu hii. Hilo ni jema, Mkristo bora. Ni wangapi watakaoinua mikono yao kwa hilo? "Nataka kuwa Mkristo bora zaidi." Mungu akubariki. Hilo ni tamu, tamu sana.

273 Unaona, unapata msingi huo, naye Mungu, kwa kuwa tunajaribu kuwaleta watu Kwake, hiyo itamfanya arudi kesho usiku na sehemu maradufu, mnaona, tunapomthibitishia ya kwamba sisi ni waaminifu katika kujaribu kufanya yote tuwezayo, tukiamini yale ambayo ametufanyia. Mnaamini yale . . . Imekuwa ni Mungu anayefanya mambo haya? Mnaona, tunataka kulikubali, kulikumbatia kwa moyo wetu wote, na kusema, "Bwana Yesu, nakupenda."

274 Sasa, iwapo mtaendelea tu kuamini hivyo, mtaona mambo yakitokea ambayo hamkufikiria yangetokea. Mnaona? Angalieni tu kitakachotendeka. Piga simu tu mahali fulani umwalike mtu fulani.

275 Sasa, ninyi nyote, ninawatakeni, kwamba mvulana huyu, aliyesimama kule nyuma kumkubali Kristo kama Mwokozi Wake, nataka baadhi yenu Wakristo mhakikishe ya kwamba kijana huyo anamfikia mhudumu mara moja na kujiandaa, sababu . . . kwa ajili ya ubatizo, na chochote kile, kumpokea Roho Mtakatifu sasa.

276 Nanyi nyote sasa mnaoamini hilo, Mbele za Kristo, kwamba mnamkubali Yeye kama Mponyaji wenu, nataka msimame, kwamba mmewekeana mikono, mtu fulani amekuwekea mikono, nawe unaamini ya kwamba unaweza kumkubali kama Mponyaji wako, simama kwa miguu yako wakati huu. Angalia tu ni aina gani ya imani unayoweza kumthibitishia Mungu kwamba,

"Ninaamini." Hiyo ni kweli. Mshukuru Bwana. Vema. Amina. Ajabu hiyo.

277 Sikilizeni, enyi kanisa dogo, dumisheni imani ya namna hiyo, na mtoke mwende huku nje na kufanya kazi fulani, sasa kila mmoja wenu awe mhubiri, umlete mtu fulani. Sasa, usininii . . . Ni wangapi wanaojisikia vizuri, na kujisikia upya baada ya kuikubali? Inua tu mkono wako. Unaona, ni matendo tu ya Mungu, Mungu akifanya haya. Ninampenda kwa moyo wangu wote. Sasa, sote pamoja sasa, hebu tuimbe.

Na . . .

Sasa hebu tuinue mikono yetu tunapofanya hivyo.

. . . mpenda, nampenda
Kwani Yeye (Mungu akubariki Ndugu . . . ? . . .)
kwanza . . .

62-0718 Yesu Kristo Yeye Yule
Jana, Leo, Na Hata Milele
National Guard Armory
Salem, Oregon Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org